Leo yetu ndiyo kesho yetu

# Uelekeo

## Mfalme Charles agunduliwa kuwa na saratani



Uk. 19

| ISSN 2953-2787 | Toleo Na. 00050 | Bei Tanzania sh 1,000 | Jumatano Februari 7-13, 2024 |

### ...Mkapa angerudia kuwaita 'wapumbavu'



Uk. 12

### Faida na hatari kiafya za ulaji wa kuku wa 'kizungu'



Uk. 14

### Rushwa; tuzibe nyufa sasa tuepuke kujenga ukuta



Uk. 16

**KUMEKUCHA 'AIRPORT' MWANZA:**

# Agizo la Dk. Samia laanza kutekelezwa ndani ya wiki

> Najua haipendezi uwanja upo hapa na mazao yanayovunwa Tanzania yakasafirishwa kupitia uwanja wa ndege wa nchi nyingine; haipendezi hata kidogo

Uk. 4









Miundombinu ya kuhifadhia samaki (coldroom) kwajili ya kusafirisha kwenda nje ya nchi

# Makonda: Sitamficha Samia madudu yote ninayoyaona



Uk. 2

## ... Kupendekeza watendaji ambao ni wazembe wasilipwe mishahara

## Mil. 300/- kukamilisha ujenzi zahanati sita



Uk. 8

# Makonda: Sitamficha Samia madudu yote ninayoyaona

## >>Akemea viongozi wasiomsaidia Rais



Paul Makonda

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa, Itikadi, Uenezi na Mafunzo, Paul Makonda, amekemea tabia ya baadhi ya viongozi walioaminiwa na kupewa wizara na matokeo yake kutofanya kazi ya kumsadia Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.

Alisema badala yake, viongozi hao wamekuwa wakitengeneza makundi ya watu kuwasifia na kusababisha uzembe kufanyika kwa watendaji wa ngazi ya chini hali inayosababisha wananchi kutohudumiwa na kutopata maendeleo kwa wakati.

Aliyasema hayo jana wakati akisalimiana na kuzungumza na wananchi wa Mji Mdogo wa Laela Wilaya ya Sumbawanga Vijijini akiwa njiani kuelekea mkoani Songwe ikiwa ni mwendelezo wa ziara yake ya mikoa 20.

Alisema lazima amwambie ukweli Rais Dk. Samia kama atakuta madudu yoyote katika ziara yake.

"Mimi wala sihitaji viongozi wa Serikali wasiofanya kazi wanipende kwa madudu yao, ziara hizi tunazofanya, CCM itaweka bayana kila sekta ili kuona kazi inafanyika au la.

"Wapo baadhi ya viongozi wameaminiwa na kupewa wizara badala ya kufanya kazi walizopewa wao wanahangaika kutengeneza watu wa kuwasifia badala ya kuwasimamia watendaji wao huku chini maana mambo hayaendi vema sehemu nyingi," alisema.

Alisema haogopi kuchukiwa wala kusemwa na bahati mbaya yeye siyo mwoga kwa kitu chochote na ameapa hatamdanganya Mwenyekiti wa CCM, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akisisitiza kuwa lazima amwambie ukweli kama atakuta madudu yoyote katika ziara yake.

"Mwenyekiti wa CCM Rais Dk. Samia ametoa fedha nyingi sana kwa miradi ya maendeleo nchi nzima kwa kila wizara na kila sekta lakini baadhi ya viongozi hawasimamii kwa kufuatilia na matokeo yake wanampelekea taarifa Rais kwamba mambo yapo sawa kumbe chini huku wananchi wanateseka, hilo kwangu kupitia ziara hizi, sitalifumbia macho," alisema.



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akizungumza na Spika mstaafu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Anne Makinda, jijini Dodoma juzi.

## ...Kupendekeza wazembe wasilipwe mishahara

**Na Mwandishi Wetu, Mbeya**

KATIBU wa NEC Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa Chama Cha Mapinduzi, Paul Makonda, amesema atapendekeza kutolipwa mishahara kwa watendaji wa serikali ambao wamekuwa wazembe kukamilisha miradi mbalimbali ya maendeleo.

Alitoa kauli hiyo jana Sumbawanga Vijijini kwenye Kata ya Miangulia baada ya kukuta malalamiko ya wananchi wanaodai kutokujengwa kwa barabara ya Kavifuti kwenda Miangalua licha ya Benki ya Dunia kutoa fedha za mradi huo wakati wa bajeti ya mwaka 2022/23.

Wakati Makonda akizungumza na Meneja wa Tarura wa eneo hilo, alisema uzembe wa kutokukamilisha miradi kwa wakati, umekuwa ukiigharimu CCM kutokana na kushindwa kukamilisha ahadi kwa wananchi.

Kulingana na wananchi, Benki ya Dunia ilitoa Sh. milioni 352 kwa mwaka wa fedha 2022/23 na kufikia sasa Tarura inasema inaendelea na mchakato wa manunuzi kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo.

# Rais wa Poland kesho kutua Dar kwa ziara ya siku mbili



Rais Andrzej Duda wa Poland

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Poland, Andrzej Duda, anatarajiwa kuwasili nchini kesho kwa ziara ya kitaifa ya siku mbili.

Taarifa iliyotolewa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini jijini Dodoma jana ilisema katika ziara yake hiyo, Rais Duda atafuatana na mwenzi wake, Agata Komhauser –Duda na kupokelewa na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, January Makamba pamoja na viongozi wengine waandamizi wa serikali katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere jijini Dar es Salaam.

Taarifa ilisema ziara hii ni ya kwanza nchini kwa ngazi ya Rais na inalenga kuimarisha ushirikiano wa uwili kati ya Tanzania na Poland

Iliongeza kuwa kwa takriban miaka 62, Tanzania na Poland zimekuwa zikishirikiana kwenye miradi ya maendeleo katika sekta ya kilimo, fedha hususan masuala ya kodi, viwanda, biashara, utalii, elimu, usafiri tiba za mifugo na afya na maji.

Kadhalika, taarifa ilifafanua kuwa ziara hiyo pia inalenga kuibua maeneo mapya ya ushirikiano kupitia sekta za ulinzi na usalama, nishati, madini, ulinzi wa mitandao, utamaduni na uchumi wa buluu.

Taarifa ilisema asiku inayofuata yaani Februari 9, mwaka huu, Rais Duda atapokelewa rasmi Ikulu jijini Dar es Salaam na mwenyeji wake, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, na kuwa na mazungumzo ya faragha, mazungumzo rasmi yatakayohusisha wajumbe wa pande zote mbili na baadaye watazungumza na waandishi wa habari kuelezea waliyokubaliana katika mazungumzo yao.

Aidha, taarifa iliongeza kuwa Rais Duda anatarajia kutembelea mradi wa matibabu ya dharura katika Hospitali ya Aga Khan jijini Dar es Salaam ambao Serikali ya Poland imetoa Dola za Marekaani 1, 136, 703.71n kufadhili mradi huo.

"Mradi huu unalenga kutoa huduma kwa sekta ya matibabu na kusaidia elimu ya wahudumu wa afya katika Mkoa wa Dar es Salaam," taarifa ilisema.

# Tanroads yafanya majaribio matumizi teknolojia mbadala

**Na Mwandishi Wetu, Dodoma**

SERIKALI kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (Tanroads), imefanya majaribio ya awali ya matumizi ya teknolojia mbadala katika ujenzi wa arabara kwa baadhi ya maeneo na inaendelea kutathmini ufanisi wake kwenye mazingira kwa kutumia teknolojia hizo mpya za kisasa zinazotumia gharama nafuu.

Hayo yalielezwa Bungeni jijini Dodoma jana na Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa wakati akijibu swali la Mbunge wa Busekelo, Atupele Mwakibete, aliyehoji serikali haioni haja ya kutumia teknolojia mpya ya kisasa na gharama nafuu katika ujenzi wa barabara nchini.

Waziri Bashungwa alisema mtaalam wa ujenzi kwa kutumia teknolojia hizo, alipatikana na majaribio yatafanyika katika barabara ya Chamwino Ikulu – Babalo – Itiso (km1.1) mkoani Dodoma kwa kutumia teknolojia ya Geopolymer Stabiliser na barabara ya Mtwara – Mnivata (km 12) mkoani Mtwara kwa kutumia teknolojia ya Amarseal Surface Rejuvenator.

Alifafanua kuwa teknolojia hizo zimeanza kutekelezwa na Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (Tarura) ambapo wataalamu walieleza zimekuwa na manufaa katika barabara ambazo zinapita magari yasiyo na uzito mkubwa.

# Mwenyekiti Kamati ya Ujenzi wa shule kortini

**Na Mwandishi Wetu, Morogoro**

MWENYEKITI wa Kamati ya Ujenzi wa Shule katika Kijiji cha Mlilingwa mkoani Morogoro, Suleiman Mwishehe, amefikishwa mahakamani kwa tuhuma za kujaribu kumhonga Sh. milioni tatu Afisa wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (Takukuru) ili asishtakiwe kwa ubadhirifu wa Sh. milioni 90 za ujenzi.

Mkuu wa Takukuru Mkoa, Manyama Tungaraza, alisema mtuhumiwa huyo alikamatwa kwenye Ofisi za Takukuru alipokwenda kupeleka kiasi hicho cha fedha kati ya Sh. milioni tano alizoshawishi awali kuwa atatoa ili asifikishwe mahakamani.

Mtuhumiwa alifunguliwa kesi ya ubadhirifu wa Sh. milioni 90 zilizoidhinishwa na kuingizwa kwenye akaunti yake binafsi kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya walimu na chumba cha darasa ambapo ameshindwa kukamilisha kazi hiyo hadi sasa.

# Mke: Talaka anipe, lakini watoto aniachie

**Na Zawadi Kapambwe, Mbeya**

MKE aliyefikishwa mahakamani katika kesi ya madai ya talaka, ameiambia Mahakama kuwa yupo tayari kuipokea, lakini kwa sharti la mumewe amuachie watoto.

"Mheshimiwa Hakimu, huyu bwana alishatutelekeza muda mrefu mimi na wanangu, hapo alipo, ana mke mwingine na watoto, anataka kurudisha mbavu kwangu baada ya kumuacha mke mdogo," alidai Mariam David (40), mkazi wa Mabatini jijini hapa mbele ya Hakimu Nitike Kiputa, wa Mahakama ya Mwanzo Mjini jijini Mbeya.

Kwa mujibu wa Mariam, migogoro kati yake na mumewe, ilianza baada mumewe kupata mwanamke mwingine.

"Wakati akiishi na mke mdogo, alipata ajali mbaya na ndipo mke mdogo alipomtupia vitu vyake nje naye akaamua kurudisha miguu yake kwangu," alidai Mariam.

"Kiukweli, huyu bwana mimi siwezi hata kurudiana naye, hapo alipo hawezi hata kufanya tendo la ndoa, ajali aliyopata iliharibu nyonga, sasa kama alivyokuwa mzima aliniona mimi siendani naye na kuamua kuoa, hivyo arudi tu kwa mke wake, mdogo," alisisitiza Mariam.

Awali, mdai Fredy Edson (43), alifika mahakamani akiomba mahakama kuvunja ndoa yake kwa madai kuwa mkewe amekuwa akirudia usiku wa manane na wakati mwingine harudi kabisa.

Kesi hiyo iliahirishwa hadi Februari 12, mwaka hu itakapotolewa hukumu.

> **Kiukweli, huyu bwana mimi siwezi hata kurudiana naye, hapo alipo hawezi hata kufanya tendo la ndoa, ajali aliyopata iliharibu nyonga.**

# Maambukizi VVU yapungua

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu, amesema maambukizi ya VVU nchini, yamepungua kutoka asilimia saba mwaka 2003/2004 hadi kufikia asilimia 4.4 mwaka 2022/2023, kukiwa na tofauti kati ya watu na maeneo mbalimbali ya kijiografia.

Katika taarifa iliyotolewa kupitia mtandao wa kijamii wa Instagram wa wizara hiyo ilieleza kuwa Waziri Ummy aliyasema hayo jijini Dar es Salaam wakati akifungua mkutano wa siku mbili wa mapitio ya kimkakati wa PEPFAR COP muhula wa 23 kwa lengo la kutathmini hatua iliyofikiwa kuhusu mwitikio wa VVU katika kufikia udhibiti wa Ukimwi ifikapo mwaka 2030.

"Kikao hiki kinalenga kujadili na kubainisha mikakati itakayowezesha ufanisi wakati wa utekelezaji wa afua za msingi na kubainisha ufanisi utakaowezesha kufikia malengo kabambe yaliyoainishwa katika sera na nyaraka za kimkakati za nchi," alisema Waziri Ummy.

Aidha, Waziri Ummy alisema kupaumbele katika masuala ya VVU/Ukimwi ni pamoja na kulinda mafanikio yaliyofanyika, kupunguza maambukizi mapya husussan kwa vijana balehe pamoja na kupunguza maambukizi mapya kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto.

Alisema Tanzania imepiga hatua kubwa katika nyanja mbalimbali za mwitikio wa VVU ambapo kwa mujibu wa ripoti ya UNAIDS 2022, Tanzania imefikia Mkakati wa Kimataifa wa Ukimwi 2021 hadi 2026 kwa lengo la matibabu.

"Mafanikio haya yamechangiwa na matokeo ya Utafiti wa Athari za VVU Tanzania mwaka 2022-2023 (HII 2022-2023) ambao uliripoti kufikiwa kwa malengo ya UNAIDS 95-95-95 kwa asilimia 82.7, 97.9 na asilimia 94.3 (ngazi ya jamii)," alisema Waziri Ummy.

"Ikijumuisha asilimia 95 ya watu wanaokadiriwa kuwa na maambukizi ya VVU na wanafahamu hali zao za VVU, asilimia 95 ya walioambukizwa VVU na wanatumia dawa za kufubaza VVU (ARVs) na asilimia 95 ya wale wanaotumia ARVs walifikia hali ya kufubaza VVU," alifafanua Waziri Ummy.

Aidha, Waziri Ummy aliwashukuru washirika wa kimataifa wakiwemo PEPFAR, Global Fund, UNAIDS, WHO, UNICEF, CDC, USAID, DOD pamoja na Peace Corps kwa msaada usioyumba wa kiufundi na kifedha katika azma ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kumaliza janga la VVU na Ukimwi ifikapo mwaka 2030.



Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu.



Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi, akiwa kwenye picha ya pamoja na Balozi wa Angola, Sandro de Oliveira (kushoto pichani), Balozi wa Msumbiji, Balozi Ricardo Mtumbuida (kulia pichani) na Balozi wa Afrika ya Kusini, Noluthando Mayende-Malepe (kushoto kwa Dk. Nchimbi), baada ya mazungumzo kuhusu masuala mbalimbali, Februari 5, mwaka huu Ofisi Ndogo ya Makao Makuu ya CCM, Lumumba, jijini Dar es Salaam.

# Agizo la Samia laanza kutekelezwa

**Na Mwandishi Wetu**



**Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Amos Makalla (kulia), akiwa kwenye kikao na Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, Masha Mshomba na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA), Mussa Mbura, Makao Makuu ya NSSF, jijini Dar es Salaam juzi.**

AGIZO la Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, alilotoa kwa Mkuu wa Mkoa wa Mwanza Amos Makalla, limeanza kutekelezwa ndani ya wiki moja.

Januari 30, mwaka huu, Rais Dk. Samia akizungumza na wakazi wa mkoa huo baada ya kugawa boti na vizimba kwa wavuvi wa Kanda ya Ziwa, alimtaka Mkuu wa Mkoa, kufuatilia kufanya maboresho ya Uwanja wa Ndege wa Mwanza kwa kuweka jengo jipya la abiria na miundombinu ya kuhifadhia samaki (coldroom).

Alimtaka Mkuu wa Mkoa kuhakikisha kwamba Uwanja wa Ndege wa Mwanza, unatumika kusafirisha mazao ya uvuvi na mengine.

"Najua haipendezi uwanja upo hapa na mazao yanayovunwa Tanzania yakasafirishwa kupitia uwanja wa ndege wa nchi nyingine; haipendezi hata kidogo," Rais Dk. Samia alisisitiza.

Aidha, alitoa maelekezo kuhusu ujenzi wa jengo la abiria na uendelezaji wa uwanja huo.

Katika utekelezaji wa maelekezo ya Rais Dk. Samia, Mkuu wa Mkoa, Makalla, ameibukia kutangaza fursa zinazopatikana katika uwanja huo huku akiualika Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) kuwa mbia muhimu wa uwekezaji katika uwanja huo.

Makalla alitoa mwaliko huo katika kikao na Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, Masha Mshomba na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA), Mussa Mbura, Makao Makuu ya NSSF, jijini Dar es Salaam juzi.

Alizitaja fursa za uwekezaji zilizopo kuwa ni kuuendeleza uwanja huo kwa kuboresha jengo la abiria, pia kujenga jengo kubwa la abiria ambalo litakuwa na hadhi ya kimataifa, kuboresha njia ya kutua na kuruka ndege, kuboresha mfumo wa taa za kuongozea ndege pamoja na kujenga hoteli ya kitalii yenye hadhi ya nyota tano.

Aliushukuru mfuko huo kwa kuonesha nia hiyo pamoja na TAA kuwa tayari kuwakaribisha NSSF katika uwekezaji na kuona utayari wa taasisi hizi mbili za Serikali kufanya kazi kwa pamoja ili kukuza uchumi na kuleta maendeleo.

"Tunawakaribisha wadau wengine kwa sasa kipaumbele tumeanza na NSSF kwa sababu tayari wameshawekeza katika mradi wa jengo la hoteli ya nyota tano na sisi Mkoa wa Mwanza, tunawashukuru kwa sababu tuna mkakati wa kukuza utalii katika jiji letu, pamoja na mambo mengine NSSF tayari wameonesha nia ya dhati ya kuendelea kuwekeza katika Mkoa wa Mwanza," alisema.

Naye, Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, Mshomba alimshukuru Mkuu wa Mkoa Makalla kwa kuwa na kikao na taasisi hizo ambacho kimezungumzia mambo mbalimbali ikiwemo kutoa kipaumbele kwa NSSF kuwa mwekezaji mkuu katika kuendeleza Uwanja wa Ndege wa Mwanza.

"Tunaendelea kumshukuru Rais Dk. Samia kwa jinsi ambavyo ameendelea kufungua nchi na kutuletea fursa za wawekezaji ambao kwetu sekta binafsi ni muhimu kwa kuandikisha wanachama na kukusanya michango," alisema.

Alisema NSSF kwa kushirikiana na TAA, watafikia hatua ya makubaliano na hatimaye waendelee katika hatua ya utekelezaji kwa maeneo waliyoyabainisha ambayo yataleta faida katika uwekezaji wa mradi huo kwani lengo ni kujenga uchumi wa nchi.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa TAA, Mbura alisema mamlaka hiyo imewasilisha fursa mbalimbali kwa NSSF ili washirikiane kuwekeza katika Uwanja wa Ndege wa Mwanza.

Alisema TAA pia inamshukuru Rais Dk. Samia kwa kuiagizwa kufanya maboresho katika Uwanja wa Ndege wa Mwanza kwani tayari fedha kwa ajili ya maboresho hayo, zimeshafika na hivi punde wataanza ukarabati wa jengo hilo.

Mkoa wa Mwanza ni miongoni mwa mikoa ambayo iko karibu na Hifadhi za Taifa, ikiwemo Hifadhi ya Taifa ya Serengeti, kupitia Mwanza ambapo inamchukua mtalii saa moja awe ametoka nje ya nchi au ndani ya nchi kwenda Serengeti kutalii na kurudi Mwanza.

Kadhalika, Mkoa wa Mwanza ni moja ya mkoa nchini Tanzania ambao una shughuli nyingi za kiuchumi ikiwemo uvuvi, kilimo, madini, utalii na biashara, hivyo kuwepo kwa mzunguko mkubwa wa watu na kuufanya Uwanja wa Ndege wa Mwanza kuwa na watumiaji wengi.

## Watoto 300 waliofanyiwa ukatili wapatiwa matibabu

**Na Mwandishi Wetu, Morogoro**

WATOTO 300 waliobainika kufanyiwa vitendo vya ukatili katika maeneo mbalimbali ya Manispaa ya Morogoro, wamepatiwa huduma kutoka Kituo cha Pamoja cha Huduma ya Mkono kwa Mkono kwa Watoto waliofanyiwa ukatili kilichopo chini ya Chuo Kikuu kishiriki cha Jordan mkoani Morogoro.

Akizungumza na waandishi wa habari mkoani Morogoro jana, Mwanasheria wa kituo hicho, Agnes Ngussa, alisema watoto hao waliofanyiwa vitendo hivyo vya ukatili, wamepatiwa huduma za afya kulingana na uhitaji, kisaikolojia/unasihi huku waliofanya vitendo hivyo, wakifikishwa kwenye vyombo vya kisheria.

Ngussa ambaye pia ni Mratibu Msaidizi wa kituo hicho, alisema kutokana na kukithiri kwa vitendo vya ukatili dhidi ya watoto, wameamua kutoa elimu kwa watoto 5,000 katika shule 67 za kata 15 zilizopo Manispaa Morogoro mkoani hapa.

Alisema lengo la kutoa mafunzo hayo, ni kuhakikisha elimu hiyo walioipata kuhusu ukatili inafikishwa na kuisambazwa kwa watoto wenzao katika jamii inayowazunguka.

Akizungumzia vitendo vya ukatili dhidi ya watoto, Mratibu wa kituo hicho, Dk. Getrude Lebby, alisema moja ya sababu inayochangia watoto kufanyiwa vitendo vya ukatili, ni baadhi ya familia kuwapa watoto majukumu yasiyo yao ikiwemo kufanya biashara mbalimbali.

## DMDP kuunganisha Temeke, Mkuranga

**Malengo ya Serikali ni kuziunganisha Wilaya za Temeke na Mkuranga, mpaka sasa maeneo matatu ya Kilwa, Tambani na Rufu Nampombo yameunganishwa kwa madaraja na makalavati na yanapitika kwa mwaka mzima.**

**Na Mwandishi Wetu, Dodoma**

KATIKA jitihada za kuendelea kuwaunganisha wananchi wa Wilaya mbili za Temeke na Mkuranga, Serikali imepanga kuboresha kwa kujenga madaraja na makalavati ya Churwi, Tabowa na Majimatitu kupitia Mradi wa Uendelezaji wa Jiji la Dar es Salaam (DMDP).

Naibu Waziri Ofisi ya Rais-Tamisemi, Deogratius Ndejembi, alisema hayo wakati akijibu swali la Mbunge wa Mbagala jana, Abdallah Chaurembo, aliyehoji mpango wa Serikali katika kuziunganisha Mbagala na Mkuranga.

"Malengo ya Serikali ni kuziunganisha Wilaya za Temeke na Mkuranga, mpaka sasa maeneo matatu ya Kilwa, Tambani na Rufu Nampombo yameunganishwa kwa madaraja na makalavati na yanapitika kwa mwaka mzima. Kwa sasa serikali imepanga kuboresha kwa kujenga madaraja/makalavati ya Churwi, Tabowa na Majimatitu kupitia DMDP.

# Serikali yawabana maafisa ugani

**Na Abdul Mitumba, Ruangwa**

SERIKALI imewataka maafisa ugani kila kata na vijijji, kuwatembelea wananchi mashambani na kuwashauri namna bora ya kuendesha kilimo bora na cha kisasa ili kuzalisha mazao kwa wingi hatimaye waboreshe hali zao za maisha.

Kadhalika, Serikali imeagiza maafisa kilimo hao kusimamia kikamilifu mashamba darasa yote ili wakulima wajifunze na wahamishie ujuzi katika mashamba yao.

Maagizo hayo yalitolewa na serikali kupitia kwa Mkuu wa Wilaya ya Ruangwa, Hassan Ngoma, alipotembelea mashamba darasa na ya wakulima katika Kata za Mandawa, Mbekenyera, Namichiga, Nambiranje, Chunyu na Matambarale.

Alisema kilimo cha miaka ya hivi karibuni, kinawalazimisha wakulima kulima kisasa kwa kutumia pembejeo hasa kutokana na nchi kukumbwa na mabadiliko ya tabianchi.

"Ninyi maafisa ugani, ndiyo wamiliki wa haya mashamba darasa, kama ilivyo kwa wananchi wanavyomiliki mashamba yao, hivyo ni muhimu mkayatunza ili wakulima waige utaalam unaotumika kuendeleza mashamba yao, alisema.

Maofisa ugani wa Kata za Mandawa, Frank Shinyangwe, Saidi Namute (Chibula) na Anuari Engema (Mbekenyera), wakizungumza katika ziara hiyo, walimuahidi Mkuu wa Wilaya Ngoma kuwafikia wakulima kwa wakati na kuwapa elimu ya kanuni bora za kilimo cha kisasa.

Naye mkulima, Sabiam Lihakwa, wa Kijiji cha Namichiga akizungumza kwa niaba ya wenzake, waliwashukuru wataalam hao kwa elimu ya kilimo wanayotoa kupitia mashamba hayo darasa.

Ziara na maagizo ya Mkuu wa Wilaya kwa maafisa ugani hao vimekuja ikiwa ni takriban miezi tisa tu tangu serikali ilipowakabidhi pikipiki maafisa hao ili kufuatilia kazi za wakuma, ambapo Mkuu wa Wilaya huyo aliwaambia kazi zao zitapimwa kwa matokeo mashambani.



Mkuu wa Wilaya ya Ruangwa, Hassan Ngoma, akielekeza jambo alipotembelea moja ya mashamba darasa.




# Ndoa hii hairekebishiki tena, naivunjilia mbali - Hakimu

**Na Zawadi Kapambwe, Mbeya**

MAHAKAMA ya Mwanzo Mjini, imevunja ndoa baina ya Yusta Amenye (42) na Fuguta Mwasikusi (53), wote wakazi jijini Mbeya baada ya kujiridhisha kuwa haiwezi kurekebishika tena.

Akitoa hukumu hiyo, Hakimu wa mahakama hiyo, Upendo Moshi, alisema baada ya kusikiliza kwa kina pande zote mbili, Mahakama imegundua kuwa ndoa hiyo kamwe haiwezi kurekebishika.

"Ndoa inaunganishwa na watu wawili, yaani mke na mume, kadhalika ndoa hiyo hiyo inavunjwa na watu hao hao, yaani mke na mume," alisema Hakimu Upendo.

Awali, ilidaiwa kuwa mdai Yusta, alifika makakamani hapo kudai talaka kwa madai kuwa hajapatiwa tendo la ndoa kwa muda mrefu pia mume wake na amekuwa akimnyanyasa kila uchao.

Alidai kuwa mbali na kutopewa tendo la ndoa, mumewe amemtelekeza pamoja na watoto kwa kutopewa huduma za matunzo ikiwemo chakula, malazi na ada za watoto shuleni.

Kwa mantiki hiyo, Hakimu Upendo alivunjilia mbali ndoa hiyo yenye familia ya watoto kadhaa na kuwaambia kwamba kila mtu yupo huru kuoa ama kuolewa, lakini akamtaka mdaiwa (mume), kuhakikisha kwamba anawahudumia watoto kwa chakula, malazi na elimu.

> Mbali na kutopewa tendo la ndoa, mume wangu amenitelekeza pamoja na watoto kwa kutopewa huduma za matunzo ikiwemo chakula, malazi na ada za watoto shuleni.

# Maoni ya Mhariri & Uchambuzi

## HII NI KERO

## Chonde Tanesco



Tunajua kuna upungufu wa umeme na hivyo kuna mgao ambao hata hivyo umepungua makali katika siku za karibuni.

Lakini hivi karibuni, hususani katika eneo la Mbagala tumeshuhudia umeme ukikatika kwa siku hadi zaidi ya mara sita. Yaani unakatika sasa baada ya muda unarudi, mara unakatika unarudi, unakatika unarudi. Hali hii ni hatari katika vifaa vya umeme.

Tumesikia habari njema za mitambo ya Bwawa la Julius Nyerere kuanza kujaribiwa lakini kabla haijaanza kuchapa kazi, ni vyema nyiye Tanesco mfanye mgao kwa haki bila upendeleo lakini pia hii washa-zima washa-zima mhakikishe mnaondokana nayo.




## MAONI YA MHARIRI

# Karibu mgeni wetu, Rais wa Poland, Andrzej Duda

Tanzania inatarajia kumpokea mgeni mashuhuri ambaye ni Rais wa Poland, Andrzej Duda.

Taarifa iliyotolewa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini jijini Dodoma jana ilisema Rais Duda atakuwepo nchini kwa ziara ya kitaifa kwa siku mbili yaani Februari 08 hadi Februari 09, mwaka huu.

Ziara ya Rais Duda ambaye anafuatana na mwenzi wake, Agata Komhauser-Duda, hapa nchini, imelenga kuimarisha uhusiano wa kihistoria kati ya nchi hizi mbili.

Hii ni ziara ya kwanza nchini kwa ngazi ya Rais ambapo kwa takriban miaka 62, Tanzania na Poland zimekuwa zikishirikiana kwenye miradi ya maendeleo katika sekta mbalimbali za maendeleo.

Baadhi ya sekta ambazo Tanzania zimekuwa zilikishirikiana katika kipindi hicho ni pamoja na kilimo, fedha hususan masuala ya kodi, viwanda, biashara, utalii, elimu, usafiri tiba za mifugo na afya na maji.

Hata hivyo, ziara hii kwa sasa imelenga kuibua maeneo mapya ya ushirikiano kupitia sekta za ulinzi na usalama, nishati, madini, ulinzi wa mitandao, utamaduni na uchumi wa buluu.

Watanzania tuna matumaini makubwa na ziara hii kwa kuwa wanaamini kuwa itazidisha ushirikiano katika nyanja kadhaa za maendeleo kwa manufaa ya mataifa haya mawili.

Kama ilivyo desturi yetu Watanzania, tuungane kwa pamoja kumkaribisha na kumpokea mgeni wetu huyu ili arejeapo nyumbani kwao, akiitangaze nchi yetu kwa mazuri na hatimaye wananchi wake, wazidi kumiminika nchini kwa shughuli za kitalii na uwekezaji ili kuinua Pato letu la Taifa.

## Wasiliana nasi


| | |
|---|---|
| **Mhariri Mkuu:** +255713263775 / +255748115000 | **S. L. P:** 15110, Dar es Salaam |
| **Mhariri wa Habari:** +255768411003 | **Makao Makuu Mtaa:** Barabara ya Morogoro |
| **Mhariri Michezo:** +255787559090 | **Jengo la:** Aura Mall |
| **Meneja Masoko/Biashara:** + 255718480406 / + 255733768825 | **Chumba Cha Habari:** +255 (0)222151532 |
| | **Email:** uelekeohabari@gmail.com |


## JICHO LANGU

Na Abdul Mitumba, Ruangwa

# Vigodoro vinadumaza maendeleo Ruangwa

NAFIKIRI huu ni utamaduni mpya, maana miaka mitano hadi saba nyuma, jamii na wakazi wa Ruangwa hawakuwahi kushuhudia.

Ukifika wilayani Ruangwa, iwe mjini au vijijini sasa ni karibu kila kaya, kila familia utaishuhudia ikiwa katikati ya shughuli zinazoambatana na sherehe za ngoma na muziki, wenyewe wanaita vigodoro.

Ni aina fulani ya muziki unaotumia spika zinazotoa sauti kubwa inayoambatana na aina tofauti za muziki.

Ukifika shughulini au kusikia muziki kwa mbali, miziki inayotawala ni singeli, mchiriku, taarabu ya mwendo kasi, bongofleva na miziki ya kikongo kwa mbaaaali.

Lakini, pamoja na majina kadhaa mazuri yanatumika kama kimvuli cha uwepo wa vigodoro hivyo, kuna shida sehemu hasa katika gharama zinazotumika kuandaa na kukamilisha shughuli zenyewe.

Sababu zinazotajwa kuwepo kwa shughuli hizo ni pamoja na mahafali, kumbukizi za siku za kuzaliwa, sherehe za jando na unyago na harusi.

Lakini unaweza kujiuliza kwamba mbona mahafali huwa si yanafanyika shuleni au vyuoni tena kwa pamoja!? Lakini huku Ruangwa kwa kila mzazi au mlezi anamfanyia mwanae nyumbani kwa sherehe kubwa!

Au kama ni kumbukizi ya siku ya kuzaliwa mtoto au mtu mzima, utashuhudia muziki mnene, sare, vyakula na pombe mchanganyiko zikiwemo zinazotengenezwa kwa kutumia kimea cha mazao ya vyakula.

Pia kuna vikundi maalumu vya wanawake, lakini kibaya kwenye vikundi hivyo wanawake husutana na kupigana vijembe kiasi cha kuhatarisha amani.

Hiyo tisa, kumi utakuta katika baadhi ya mtaa kuna sherehe za unyago.

Hapo kuna vibweka chungu mzima

Nisingependa kuvisimulia lakini kwa uchache hapo utakuta pana sare, muziki mnene, vyakula na pombe. Haijalishi iwe bia, kangara,wanzuki, pombe ya mnazi au ulaka inayotengenezwa kwa kutumia mabibo.

Katika sherehe za harusi, hapa ndipo utapata kila kitu ambacho hukukiona kwenye birthday, unyago, jando na mahafali, hapo utakipata na ziada.

Inawezekana huu ni utamaduni mpya ambao wana Ruangwa wameamua kuuishi, lakini kinachoshangaza wengi ni pale inapofika Januari hadi Februari watoto hawapelekwi shule.

Au wakipelekwa ni kwa kuchelewa mno na wakati mwinge wakiwa hawana mahitaji muhimu shuleni.

> **Lakini unaweza kujiuliza kwamba mbona mahafali huwa si yanafanyika shuleni au vyuoni tena kwa pamoja!? Lakini huku Ruangwa kwa kila mzazi au mlezi anamfanyia mwanae nyumbani kwa sherehe kubwa!**

Sababu ni kwamba, wazazi wenzetu wanakuwa wamemaliza fedha na vyakula kwa kugharamia shughuli.

Cha kushangaza zaidi ni pale tunapoambiwa kuwa kuna michango ya fedha wanachangishana kupitia vikundi mbalimbali

Uwepo wa utamaduni huu umethibitishwa katika utafiti uliofanywa na mashirika ya hiari ikiwemo Asasi yangu ya Kuunganisha Vijana Kimaendeleo Ruangwa (AKUVIKIRU), ambapo tangu 2017 imekuwa ikitekeleza mradi wa Kuhamasisha Maboresho ya Elimu ya Sekondari Wilaya ya Ruangwa ambapo mradi umefika katika shule 12 za kata za wilaya ya Ruangwa.

Jicho Langu, linaona siyo sawa jamii kutumia fedha nyingi katika shughuli zisizo na matokeo ya muda mrefu katika jamii, huku watoto wakishindwa kwenda shule kwa wakati.

Hali hii, ilimlazimu Mkuu wa Wilaya ya Ruangwa, Hassan Ngoma mapema Januari mwaka huu, kutembelea shule kwa shule za kata kuhimiza watoto wafikishwe kwa wakati kauanza masomo.


Hata alipotembelea wilaya ya Ruangwa mwishoni mwa mwaka jana, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, pamoja na mambo mengine aliyosema, aliwasihi wakazi wa Ruangwa kupunguza sherehe ikiwemo vigondoro badala yake waelekeze macho na akili zao katika kusomesha watoto.

Rais Samia alilazimika kutoa agizo hilo baada ya kuambiwa kwamba hivi sasa Ruangwa, inazungukwa na neema ya madini huku mazao ya biashara ya ufuta na korosho yakizidi pia kushamiri.

# ZIARA YA KATIBU WA NEC ITIKADI, UENEZI NA MAFUNZO YA CCM, PAUL MAKONDA WILAYANI SUMBAWANGA














# Takukuru yaonya wagombea

**Na Mwandishi Wetu, Tabora**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) mkoani Tabora, imewaonya wagombea watarajiwa katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka huu, kutojihusisha na rushwa.

Mkuu wa Takukuru mkoani hapa, Mussa Chaulo, alisema hayo wakati akitoa taarifa ya utendaji kazi kwa vyombo vya habari na kubainisha mikakati ya taasisi hiyo.

Alisema moja ya mikakati ya taasisi hiyo kwa mwaka huu kuelekea kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, ni kudhibiti vitendo vya rushwa.



Mkuu wa Takukuru mkoani hapa, Mussa Chaulo.

Alisema watahakikisha elimu ya kutosha inatolewa mapema kwa wananchi wote.

Alifafanua kuwa elimu hiyo itawapa uelewa wa masuala ya rushwa ili watakapoona mgombea yeyote akitoa rushwa, watoe taarifa haraka kwa maafisa wa Takukuru ili wakamatwe na uchunguzi ufanyike na atakayethibitika kujihusisha na vitendo hivyo, achukuliwe hatua.

Alisema malalamiko yoyote yenye mrengo wa rushwa yatakayotolewa na wananchi au wagombea kabla ya wakati na baada ya uchaguzi, yatafanyiwa uchunguzi na hatua stahiki kuchukuliwa.

Alitoa wito kwa wakazi wa mkoa huo na Watanzania wote, kuendelea kutoa ushirikiano kwa taasisi hiyo ili kuhakikisha vitendo vya aina yoyote ile vya kuomba au kupokea rushwa, vinadhibitiwa katika nyanja zote ikiwemo miradi ya maendeleo.

Alibainisha kuwa licha ya vitendo hivyo kurudisha nyuma maendeleo ya jamii, pia vinafanya wananchi wasipate kiongozi bora wa kusimamia maendeleo yao na taifa kwa ujumla.

Kamanda Chaulo alisisitiza kuwa Takukuru mkoani hapa, itaendelea kutekeleza majukumu yake kama yalivyoainishwa katika Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa namba 11 ya mwaka 2007.

Aidha, alisema wataendelea kushirikiana na wadau ili kuhakikisha vitendo vya aina yoyote vya kuomba au kupokea rushwa, havijitokezi katika jamii.

# Soko la Mbuyuni lateketea kwa moto

**Na Mwandishi Wetu, Kilimanjaro**

SOKO la Mbuyuni lililoko katika Manispaa ya Moshi mkoani Kilimanjaro, limeteketea kwa moto usiku na ksababisha hasara kwa wafanyabiashara zaidi ya 2,500, wengi wao wakiwa walipata mitaji kutokana na mikopo kwa taasisi mbalimbali za fedha.

Moto huo ulianza kuwaka juzi usiku wa kuamkia jana na chanzo chake bado hakijafahamika.

Akizungumza katika tukio hilo na kujionea hasara hiyo, Katibu wa Siasa na Uhusiano wa Kimataifa (SUKI) na Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM (MCC), Rabia Abdallah Hamid, alisema Chama chake kitakwenda kuzungumza na taasisi za benki ambazo zimewakopesha wafanyabiashara wa soko hilo kuhakikisha hawanyanyasiki katika kuirudisha.

"Viongozi mnapaswa muanze mara moja kuwatambua wafanyabiashara wangapi wanaodaiwa mikopo na kuwaorodhesha kwani kuna utaratibu wa kurejesha marejesho kila mwezi, lakini kwenye hili, sisi CCM tunakwenda kukaa na taasisi hizo ili kuhakikisha wafanyabiasha hawa hawanyanyasiki katika kipindi hiki," alisema Rabia.



# Aliyeomba msaada kwa Rais aanza tiba Bugando



Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu.

**Na Mwandishi Wetu, Mwanza**

BALTAZARI Thobias (18) mkazi wa Wilaya ya Ukerewe, mkoani Mwanza, aliyeomba msaada wa matibabu kutoka kwa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, amepokelewa katika Hospitali ya Rufaa ya Kanda Bugando kwa ajili ya uchunguzi na matibabu ya uvimbe anaomsumbua kwa miaka minne sasa.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, alitoa maelekezo ya Thobias kupelekwa Bugando, baada ya kumuomba Rais msaada wa matibabu kutokana na uvimbe huo.

Bingwa wa magonjwa ya uso, shingo, taya, kinywa na meno (Maxillofacial Surgeon), Dk. Emmanuel Motega, alisema tayari wamempokea mgonjwa huyo.

"Tumempokea Thobias, tumeanza kumfanyia vipimo vya awali vinavyohusu uchunguzi wa maradhi yake na baadaye ataonwa na jopo la madaktari bingwa kutoka idara tofauti," alisema Dk. Motega.

# NHIF: Wananchi wapuuzeni matapeli hawa

**Na Hellen Mwango**

MFUKO wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), umewatahadharisha wananchi kuwepo kwa taarifa za upotoshaji kuhusu utaratibu wa usajili wa watoto kupitia mpango wa Toto Afya Kadi ikidaiwa kwamba gharama za usajili wake ni Sh. 35,780 kwa mwaka na 95,780 kwa miaka mitano.

NHIF imeeleza kwamba taarifa hizo si za kweli na zipuuzwe.

Taarifa iliyotolewa na Meneja Uhusiano NHIF, Anjela Mziray, ilisema kuwa taarifa hizo ni za upotoshaji na kwamba mfuko huo haupokei usajili wa wanachama kwa njia ya mtandao wa WhatsApp wala michango yake kupitia namba ya simu ya mkononi na hata viwango vilivyoainishwa, pia ni vya kuipotosha jamii.

Alisema mfuko unaendelea kuwasajili watoto kujiunga na mzazi/wazazi wao kupitia Vifurushi vya Bima ya Afya huku michango yao ikitegemea na uchaguzi wa kifurushi husika na idadi ya wanaojiunga.

Taarifa iliongeza kuwa mfumo mwingine ni kupitia usajili wa jumuiya ya wanafunzi shule wanazosoma watoto baada ya mawasiliano ya mzazi/wazazi na uongozi wa shule husika kuwasiliana na ofisi ya NHIF iliyo karibu kukamilisha usajili huo unaogharimu Sh. 50,400 kwa mwaka.

"Tunawasisitiza wananchi, michango ya wanachama inalipwa kupitia namba ya malipo ya serikali inayotolewa na Mfuko baada ya kukamilisha usajili na si vinginevyo," ilisisitizaz taarifa.

Ilisema mawasiliano kati ya wananchi na NHIF, yanafanyika kwa kutumia mfumo rasmi uliowekwa na Mfuko ikiwamo namba ya huduma kwa wateja 199.

# Mil. 300/- kukamilisha ujenzi zahanati sita

**Na Mwandishi Wetu, Njombe**

JUMLA ya Sh. milioni 300 zinatarajiwa kukamilisha ujenzi wa zahanati sita katika Halmashauri ya Wilaya ya Njombe kwa mwaka wa fedha 2024/25 ili kutatua changamoto ya matibabu kwenye maeneo yasiyo na vituo vya kutolea huduma za afya.

Kwa mujibu wa Katibu wa Afya wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, Domina Kusuva, tayari bajeti ilishatengwa kukamilisha ujenzi wa zahanati hizo.

Naye Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, Valentino Hongoli, alimuagiza Mkurugenzi kukamilisha kwa haraka miradi hiyo ili kupunguza adha kwa wananchi kusafiri umbali mrefu kufuata huduma za afya.



Katika makisio na makadirio ya rasimu ya bajeti ya mwaka wa fedha wa 2024/25 yaliyosomwa na Lwidiko Mella ambaye ni Ofisa Mipango wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, kiasi cha Sh. bilioni 33.6 ikiwa mapato ya ndani na Sh. bilioni 4.1, zinatarajiwa kwenda kupunguza changamoto katika miradi viporo inayolalamikiwa kwa muda mrefu ukiwemo wa mradi wa Kituo cha Afya Mtwango.

Katibu Tawala Wilaya ya Njombe, Agatha Mhaiki, alisisitiza suala la usafi ili kujikinga na magonjwa ya mlipuko na ya kuambukizwa.


Jarida hili haliuzwi

*Leo yetu ndiyo kesho yetu*

Uelekeo

# JARIDA Jungu Kuu

| Jumatano Februari 7-13, 2024 |




UK. 12 & 13

# Kwa hili Mkapa angerudia kuwaita 'wapumbavu'

Siasa



# Waliosemwa wamechoka 2013, bado wapo Chadema - 3

**Na Mwandishi Wetu**

TUNAENDELEA kujikumbusha yaliyokuwemo kwenye waraka wa Mkakati wa kudai Mabadiliko ndani ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), leo tukiingia wiki ya tatu.

Huu ni Waraka uliosambaa mitandaoni mwaka 2013 na kusababisha baadhi ya viongozi waandamizi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) waliotuhumiwa kuandaa mkakati huo kuondolewa.

Baadhi ya waliofukuzwa ni aliyekuwa Naibu Katibu Mkuu wa Chadema, Zitto Kabwe (sasa kiongozi wa ACT-Wazelendo), aliyekuwa Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chadema Profesa Kitila Mkumbo (sasa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji) na aliyekuwa Mwenyekiti wa Chadema Mkoa wa Arusha, Samsoni Mwigamba

Baadhi ya mambo ambayo tumeangalia ni namna viongozi wa sasa walioingia madarakani 2004, walivyolalamikiwa kwa kuwa wazito kung'atuka madarakani na kupisha damu mpya kuongoza chama hicho.

Pia walidaiwa kutumia mbinu za maandamano na harakati nyingine kama Movement For Change (M4C) ambazo hata hivyo kwa majibu wa waliokuwa wakitaka mabadiliko, hazikuzaa matunda ya maana.

Tukaona kwamba licha ya mbinu hizo, Chadema hakikufanya vizuri katika chaguzi kubwa na ndogo katika kipindi cha uongozi wa viongozi hao hadi wakati waraka wa mabadiliko unaandikwa.

Pia tumeona viongozi hao wakilalamikiwa kwa ubadhirifu wa mali za chama, kukosa mbinu za kukipatia chama mapato na pia bosi kudaiwa kufanya mambo kinyume cha utaratibu. Leotunaendelea namna hii.

**DALILI ZA UFISADI**

Taasisi yetu inayo kamati ya tenda ambayo iko chini ya kamati ya makatibu na wakurugenzi. Lakini uzoefu unaonesha kwamba kamati hii haifanyi kazi. Imezimwa kimya kimya na wajumbe wote wa kamati ya tenda kwa kuwa ni wachumia tumbo wanaojigonga kwa wakuu, wamekubali kuzimwa.

Leo (2013) ikidaiwa kamati hiyo ilete nyaraka za mchakato wa manunuzi ya magari, pikipiki, vifaa vya kueneza taasisi, set ya televisheni iliyofungwa ofisini kwa mtendaji mkuu, hawana.

Manunuzi haya yote yote yanafanywa na wakuu hasa hasa mkuu wa taasisi bila utaratibu wowote jambo ambalo ni hatari na linarahisisha matendo ya kifisadi. Bila aibu, mkuu wa taasisi ndio amekuwa mnunuzi wa vifaa vyote vya chama nje ya nchi kwa bei anayoijua mwenyewe na ambaye haihojiwi popote.

Huu ni mfano wa wazi wa mgongano wa kimaslahi,jambo ambalo ni hatari kwa kiongozi mkubwa wa taasisi kama yetu inayojitambulisha katika kupinga vitendo vya ufisadi na uvunjifu wa maadili ya uongozi kwa ujumla.

Makubaliano ya kifisadi na mtu binafsi anayeuza vifaa vya kueneza taasisi. Hakuna kikao chochote cha juu kilichojadili ama kilichowahi hata kupewa taarifa tu kwamba sasa kuna mtu binafsi kapewa tenda ya kuuza vifaa vya taasisi na taasisi inanufaika vipi na mauzo hayo na kwa nini vifaa muhimu vya taasisi vinauzwa. Jambo hili linajulikana kwa wakuu tu.

Mifumo ya uteuzi wa maofisa wa makao makuu ya taasisi imevurugwa na siku hizi wakuu wa taasisi hasa mtendaji mkuu anateua na kutimua ofisa anavyotaka na mara nyingi bila hata kamati ya makatibu na wakurugenzi kujua. Mambo haya yanafanyika mbele ya macho na masikio ya mkuu wa taasisi jambo ambalo linazidi kuthibitisha kwamba mkuu na mtendaji mkuu wanajuana na wanafanya kwa kulindana.

**NANI TUMUUNGE MKONO KUCHUKUA NAFASI YA MKUU:**

Baada ya utangulizi huo unaoonyesha kinagaubaga kwamba tunahitaji mabadiliko, hatua iliyofuata ilikuwa ni kuangalia nani anaweza kuleta mabadiliko tunayohitaji. Ni vema ikazingatiwa kwamba mtu ambaye tungemuunga mkono lazima awe ni mtu mwenye uwezo mkubwa kuliko tunayetaka kumtoa. Awe ana qualities za kiuongozi na zaidi sana awe na uwezo wa kupambana na mkuu aliyeko.

Tukileta mtu asiyefahamika sana kwenye mifumo ya taasisi yetu hata kama angekuwa mzuri kiasi gani hatachagulika na mkuu aliyeko atarudi kwa urahisi na kuendelea kuididimiza taasisi.

Katika kuchunguza ndani ya taasisi tuliridhika kwamba mtendaji mkuu msaidizi (Zitto Kabwe) ana sifa zote tulizozitaja hapo juu ingawa kila mwanadamu ana udhaifu wake. Ni dhahiri pia kwamba udhaifu wa mtendaji mkuu msaidizi unarekebika kuliko wa mkuu aliyepo. Kwa ujumla mtendaji mkuu:

Ni kiongozi anayeweza kuongoza taasisi bila kujenga makundi akijali zaidi kazi ya taasisi kuliko maslahi binafsi.

Ameonesha kwa vitendo kwamba hana maslahi binafsi kwa kuwa tumeshuhudia akifanya kazi nyingi za taasisi bila kudai malipo kwa njia ya posho ama vinginevyo.

Anaheshimika na viongozi wa ndani na nje ya taasisi jambo ambalo ni la muhimu sana kwa ustawi wa taasisi na kwa yeye kuwa mkuu wa taasisi tunatarajia wakubwa wengi sana kutoka nje ya taasisi yetu kuiamini na hata kujiunga nasi katika kuhakikisha tunafanikisha lengo la taasisi.

Ni msomi wa kiwango cha juu na mwenye uwezo mkubwa katika kuchanganua mambo ya kiuchumi, kisiasa, kijamii, kimichezo, nk jambo ambalo ni muhimu sana kwa kuwa ni hatari kuwa na kiongozi asiye na ujuzi wa kutosha kwenye masuala kama hayo.

Ndani ya taasisi anakubalika kwa makundi yote ya vijana, wazee na akina mama.

Exposure kubwa na kukubalika katika siasa za kimataifa. Tunahitaji kiongozi ambaye anazifahamu siasa za kimataifa na anayeweza kuungwa mkono na viongozi wengi wa kimataifa. Ni hatari kutegemea utaweza kufanikisha malengo kama ya taasisi yetu bila mpango kabambe wa kuungwa mkono na jumuia ya kimataifa.

Mpaka hivi sasa hakuna mpango wowote wala hata mchakato wa maana kuwa connected na jumuia ya kimataifa. Kiongozi wetu mkuu wa sasa yupo 'too local' na hana mawasiliano yeyote ya maana na viongozi wengine katika kanda na kimataifa. Ndio maana mkuu huyo na mtendaji wake mkuu wamekuwa hawaonekani katika matukio makubwa ya kimataifa.

Hata katika kutoa maoni katika mambo makubwa ya kitaifa na kimataifa viongozi hawa hawapo. Kwa kifupi kwa sababu ya aina ya viongozi tulio nao, nafasi ya taasisi yetu katika nyanja za kimataifa haipo!

Aina na staili ya uongozi wa sasa wa taasisi yetu ni kina kwamba nchi hii haipo hadi taasisi yetu itakapochukua dola. Yaani tunafanya mambo kama kwamba tutaanza upya kabisa tukichukua dola. Ni kwa sababu tumegombana na kila mtu katika utawala wa nchi, vikiwemo vyombo vya ulinzi na usalama.

Ukweli ni kwamba tutavihitaji vyombo hivi kabla na baada ya kuingia madarakani na ni ndoto kudhani kwamba tutakabidhiwa nchi kwa kugombana na kila mtu. Ni kwa sababu ya mtazamo kama huu ndio maana wakuu wetu wa sasa hawaonekani kabisa katika shughuli za kitaifa kama vile sherehe za uhuru wan chi, n.k.

Uwezo wa kuwaunganisha wasomi wa kada mbalimbali, wafanyabiashara wakubwa, watumishi wa umma na sekta binafsi, nk katika kupata muunganiko wa mawazo na kutoka na sera murua zinazogusa kila sekta. Hili la kuwashirikisha litaenda sambamba na kutoa elimu kwa wote waelewe na watuunge mkono.

Tunasema hivi kwa kuwa watu wa kada mbalimbali hawajaelewa sera zetu juu ya mambo yanayowahusu mfano wafanyabiashara wakubwa, wawekezaji, wakulima, watumishi, wanafunzi,nk na hivyo hawajawa tayari kutuunga mkono. Kile kinachofanywa wakati wa uchaguzi kwa njia ya ilani ya uchaguzi na elimu kutolewa kwa njia ya kampeni majukwaani hakitoshi.

Tunahitaji watu wajue tumeunda think tank kwa ajili hiyo na baadaye wajue nini kimetokana na think tank hiyo ili wajadili na kutoa maoni na hatimaye tutoke na kitu kinachokubalikwa na wananchi wote. Na tuna imani hilo tunayempendekeza ana uwezo nalo.

Kubwa zaidi ni kwamba alishaiangalia taasisi yetu na kuona mambo yanayohitaji mabadiliko na kujiangalia yeye na kuridhika kwamba atawеza kuleta mabadiliko tunayoyahitaji na ndipo mwaka 2009 aliamua kujitosa kuutafuta ukuu wa taasisi yetu kabla ya kuombwa kumwachia aliyepo.

*Itandelea*



Hamisi Kibari

TUKUBALIANE KUTOKUBALIANA

Simu: 0758143457

# Vipo visababishi na mbinu nyingi kukomesha mimba shuleni

"KWA sasa hali imebadilika sana baada ya ujio wa daladala na bajaji. Sijafanya utafiti wa kina lakini naamini hali si kama ilivyokuwa zama zile ambazo usafiri pekee ulikuwa ni wa bodaboda."

Hayo ni maneno ya kutia faraja kutoka kwa Fazel Janja, mwandishi wa habari mkongwe pale Musoma Mjini, nilipozungumza naye hivi karibuni.

Alikuwa alijibu swali langu nililotaka kujua kama vijana wanaoendesha pikipiki za abiria, maarufu bodaboda, wanaendelea kuwa tishio la kuwapa mimba watoto wa shule katika mji huo wa kando ya Ziwa Victoria ama la.

Janja alifafanua kwamba kwa sasa watoto wengi wanaosoma shule za sekondari zilizo nje ya mji huo, hususani zilizo kando ya barabara ya Mwanza - Musoma wanakwenda shuleni asubuhi kwa kutumia mabasi ya abiria na mara nyingi hurudi na mabasi hayohayo.

"Kuna mabasi yanayokwenda hii njia ya Mwanza - Musoma madereva wake wengi ni waungwana sana. Huwa wanachukua wanafunzi pale stendi ya Musoma Bus asubuhi na kuwashusha kwenye shule zao. Jioni pia wanaporudi wanawasaidia wanafunzi usafiri," anasema Janja.

Hatua hiyo ya watoto wa shule, hususani wa kike kutumia usafiri wa mabasi, daladala na bajaji, Janja anasema umesaidia sana kupunguza wimbi la mimba shuleni zilizokuwa zikichangiwa na madereva wa bodaboda!

Miaka takribani 13 iliyopita nilipotembelea mji huo, nilikuta kilio kikubwa kwa wazazi kuhusu mimba za watoto wa shule huku vijana wanaoendesha bodaboda ndio wakinyooshewa kidole.


Mambo yalikuwa hivi miaka 13 iliyopita: Nilifika Musoma kwa ajili ya mapumziko ya wiki mbili na kufanikiwa kutembelea vijiji vya Mugango, Bwai, Nyakiswa na Wanyere ambako nilijionea mengi, mazuri na machache yenye kutia ukakasi.

Lakini nikiri pia kwamba moja ya kitu kilichofanikisha kwa haraka sana mambo yangu ni usafiri wa bodaboda.

Nikiri pia kwamba mara nyingi nilikuwa ninalazimika kuwa mkali kwa madereva wa bodaboda kwa sababu baadhi yao walionekena dhahiri hawajaiva sawasawa katika fani ya udereva.

Kwa mfano, kuna huyu mmoja ambaye nilipanda pikipiki yake kutoka Kamunyonge kuelekea Barabara ya Mukendo lakini nikalazimika kushuka kabla sijafika mwisho wa safari yangu kwa sababu nilishaona anafanya maamuzi ya ajabu na hasa nilihofia kama atamudu kukatiza vyema barabara ya Nyerere yenye magari mengi, pikipiki, watembea kwa miguu na basikeli ili kuingia upande wa pili.

Nikalazimika kutembea kwa zaidi ya mita 500 zilizobakia kuliko 'kuchezea' roho yangu na ya kwake!



Kimsingi, kama ilivyo miji mingine mingi nchini, Musoma mjini kuna pikipiki nyingi sana kiasi kwamba wakati mwingine zinakuwa kero kwa watembea kwa miguu!

Ukiachilia mbali tatizo la madereva kutokuwa na weledi mzuri wa kazi hiyo kiasi cha kuhatarisha maisha ya abiria na watu wengine wanaotumia barabara, ukweli unabaki kwamba pikipiki zinasaidia sana suala la usafiri.

Siku hizi tunaona kawaida lakini kumbe enzi zetu sisi vijana wa zamani tulioishi zama ambazo ukiona pikipiki basi ujue ni ya padri kama siyo Afisa Elimu wa Mkoa, tulikuwa na shida sana. Sehemu kubwa tulilazimika kutembea kwa miguu.

Tena mtu anaweza kukwambia "unaenda kile kijiji, si mbali. Ukifika kwenye ile milima unaona kijiji. Si mbali kabisa."

Sasa nenda uone kazi! Ukifika kwenye hiyo milima, utaangalia hadi upeo wa macho yako huoni kijiji na kudhani umekosea njia. Ukiuliza wapita njia, unaambiwa bado una kilometa kadhaa za kuchanganya miguu hadi kuanza kuona kijiji husika. Siyo kufika!

Kingine nilichokigundua wakati ule (miaka 13 iliyopita) ni waendesha pikipiki wa Musoma kusumbuliwa sana na askari polisi na hapa simaanishi wale wa usalama barabarani pekee bali hata askari aliyevaa kiraia.

Tuyaache hayo. Ninachotaka kusema ni kwamba katika muda huo mfupi niliofanya 'utalii wa ndani', nilisikia mimba za wanafunzi watano, mmoja akiwa ndugu yangu, na wote wakiwa wameponzwa na lifti za vijana wa kiume wanaoendesha bodaboda.

Freeman Nyamandege, mwendesha bodaboda wa mjini Musoma na ambaye ni mtu mzima kiasi, aliniambia wakati ule kwamba vijana wengi wanaoendesha bodaboda wakiwemo hata watu wazima, wanatumia usafiri katika kuwarubuni watoto wa shule na hata kuvunja ndoa za watu.

"Ni kweli, kuna vitendo vingi sana vya uasherati kwenye biashara hii ya bodaboda. Kuna wanaojali kazi hii wakilenga maendeleo yao lakini wapo wajinga ambao pia ni wengi tu. Wapo watu wameacha kuendesha magari na kuja kwenye pikipiki lakini wanachokitafuta si maslahi bali wamegundua kuna urahisi wa kuwapata wanawake. Amini usiamini," akasema Freeman.

Akakiri pia baadhi ya waendesha pikipiki kuwarubuni wanafunzi wanaosoma, hususani katika sekondari za kutwa na kujikuta wamewapa mimba wasizozitarajia na hasa kwa vile wengi bado ni watoto na akili hazijapevuka kiasi cha kung'amua hatari ya kushiriki mapenzi, baada ya kuhakikishiwa usafiri.

Mwandishi Fazeel Janja, ambaye wakati huo alikuwa ameshiriki katika ziara ya waandishi wa habari ya kutembelea shule zilizoko katika Manispaa ya Mji wa Musoma, alikiri kwamba waendesha bodaboda walichangia sana katika tatizo la mimba mashuleni.

Janja ambaye baada ya ziara hiyo aliandika makala mbalimbali kuelezea matatizo kadhaa aliyoyaona katika shule za kata, alishauri shule za kata kujengewa mabweni ili kuwanusuru mabinti wadogo na vishawishi vya wanaume wakiwemo waendesha bodaboda.

"Baadhi ya shule hizi ziko mbali na familia wanakotoka wanafunzi. Njiani wanafunzi hawa wanakumbana na mengi wakiwemo wanaume wanaowarubuni kwa pesa na usafiri ili wafanye nao mapenzi. Kwa vile wasichana hawa huwa pia wamefikia umri wa balehe baadhi hujikuta wakishawishika kufanya mapenzi bila kinga na kupata mimba ama hata magonjwa ya zinaa ukiwemo ukimwi," alisema Janja.

Mbali na kushauri ujenzi wa mabweni kwa ajili ya watoto wa kike, pia wakati ule nakumbuka Janja alipendekeza kwa serikali kuona uwezekano wa shule za kata kuwa na mabasi yao ili kuwachukua na kuwarudisha wanafunzi majumbani.

Alisema kingine kinachochangia mimba kwa wanafunzi ni njaa sambamba na umaskini wa wazazi. Kwa suala la njaa alishauri serikali kutoa chakula mashuleni kwa sababu mbali na usafiri, waendesha bodaboda pia huwalaghai mabinti kwa vyakula. Alisema wazazi pia wanaweza kushiriki kuchangia chakula shuleni.

Janja aliilaumu Serikali wa kushindwa kuwaondolea umaskini wa kutisha wananchi. Aliamini kama mzazi ana uwezo kifedha inasaidia sana kwa sababu binti atapata mahitaji yake muhimu mengi na kwamba wapo wazazi wanaopokea zawadi za mabinti zao bila kuuliza zimetoka wapi kwa sababu ya umaskini.

Kuhusu waendesha bodaboda kuwa tatizo, Janja alishauri matumizi ya sheria pamoja na elimu na alitamani kuona mwendesha bodaboda ama mwanaume yeyote anayemtia mimba mwanafunzi akichukuliwa hatua kali sana ili kuwatisha wengine.

"Mitaani kuna wanawake wengi wanatafuta wanaume, sasa kwa nini umharibie mwanafunzi matarajio yake ya baadaye kwa kutumia umaskini wake na utoto wake? Hawa wanahitaji adhabu kali sana," alisema Janja na kuongeza kwamba ni vyema pia kuwapiga msasa waendesha bodaboda kuhusu madhara ya kufanya mapenzi na wanafunzi ambao wanapaswa kuwachukulia kama wadogo zao wa kuzaliwa tumbo moja.

"Semina mbalimbali zingekuwa zinaendeshwa kwa waendesha bodaboda, si kuhusiana na usalama barabarani pekee bali pia hatari ya kurubuni wanafunzi wa kike ili kufanya nao mapenzi," alisema.

Wakati tatizo la mimba zinazosababishwa na waendesha bodaboda limepungua kwa mujibu wa Janja kama si kuisha, nimeandika haya ili kuwapa mwanga watu wa maeneo mengine kama nao wana changamoto kama walilokuwa nao wakazi wa Musoma kuona wafanye nini.

Kwanza kuwaomba madereva wa mabasi kusaidia kuwapa usafiri wanafunzi alimradi nao wasigeuke kuwa waharibifu. Lakini pia kufanyia kazi ushauri wa ujenzi wa mabweni ambao kwa shule nyingi umekuwa ukifanyiwa kazi, shule kuwa na mabasi yao, wazazi kupambana na kuboresha vipato vyao, matumizi ya sheria kwa wanaowapa wanafunzi, semina elekezi kwa waendesha bodaboda na kadhalika.

Siasa

# Kwa hili Mkapa angerudia kuwaita 'wapumbavu'



**Na Hamisi Kibari**

WAKATI wa ufunguzi wa kampeni za uchaguzi mkuu wa mwaka 2015 katika Viwanja vya Jangwani jijini Dar es Salaam, Rais wa Awamu ya Tatu, Hayati Benjamin Mkapa, aliwaita wapinzani kuwa ni wapumbavu na malofa.

Akimnadi Dk. John Magufuli wakati huo akiwania urais, Mkapa alifafanua kwa nini aliwaita hivyo akisema ni kutokana na madai yao kwamba wao ndio vyama vya kuwakomboa Watanzania wakati kimsingi Watanzania walikombolewa miaka mingi na vyama vya Tanu na Afro Shirazi Party (ASP).

Mkapa alisema chama pekee cha ukombozi wa Watanzania kilichobaki ni Chama Cha Mapinduzi (CCM) ambacho ni matokeo ya muungano wa Tanu na ASP.

Kimsingi, Mkapa aliwaita wapinzani wapumbavu na malofa akikerwa na hulka yao ya kupinga kila kitu, kama vile serikali iliyoko madarakani haijafanya lolote.

Licha ya kulalamikiwa kwa kauli hiyo kali, Mkapa alirudia kuwaita wapinzani wapumbavu na malofa wakati akiwa kwenye shughuli za taasisi aliyoianzisha ya Benjamin Mkapa kutokana na wapinzani kukejeli juhudi zilizokuwa zimefanywa na serikali kwa upande wa afya.

**KINANA AJIONEA MWENYEWE**

Mwishoni mwa wiki, Makamu Mwenyekiti wa CCM Tanzania Bara, Abdulrahman Kinana hakutumia maneno makali kama ya Mkapa lakini ukiyaangalia ni kama yanathibitisha shida ya uungwana duni walio nayo wapinzani, hususani viongozi wa chama kikuu cha upinzani, Chadema.

Akizungumza na wanachama wa CCM wa Mkoa wa Dar es Salaam Kinana ameonesha kwamba viongozi wa Chadema, si wakweli (wababaishaji), hawana staha na hivyo hawaendeshi siasa za kistaarabu lakini hawaeleweki wanataka nini hasa!

Hawa ni viongozi walewale ambao mwaka 2013, walitajwa na wenzao waliotaka mabadiliko ndani ya Chadema kwamba hawawezi kukifikisha kokote chama hicho. (Gazeti hili linaendelea kuchapisha Waraka wa Mkakati wa Mabadiliko ndani ya Chadema wa mwaka 2013. Kupitia Waraka huo ni wazi kwamba viongozi waliodaiwa kuwa wababaishaji na wasio na uwezo wa kukifikisha juu zaidi chama hicho, ndio ambao bado wapo madarakani na ndio ambao wamemchefua Kinana).

**CHADEMA WASHINDWA KUSEMA UKWELI**

Akielezea kuhusu mazungumzo ya maridhiano na hatimaye kuendesha siasa za kistaarabu baina ya CCM na Chadema ambayo yamekwama, Kinana amekaririwa na gazeti la Serikali (HabariLeo) akisema kwamba Chadema kimeshapokea Sh bilioni 2.7 za ruzuku ya miaka mitatu tangu kumalizika kwa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 kutoka serikalini lakini hakiweki hadharani ukweli huo.

Anasema kitendo cha chama hicho kuomba na hatimaye kupewa fedha za ruzuku ni moja ya matunda ya maridhiano kwa kuwa tangu kumalizika kwa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020, chama hicho kiligoma kuitambua serikali kwa kukataa kupokea fedha za ruzuku.

Ingawa kwa mujibu wa HabariLeo ni kama Kinana hakulizungumzia hilo, lakini hii maana yake pia ni kwamba Chadema imeomba na hatimaye kupokea fedha za ruzuku, sehemu kubwa zikitokana na wabunge wake, hususani wa viti maalumu ambao chama hicho kimekuwa kikiwakana!

**LENGO LA MAZUNGUMZO**

Itakumbukwa kwamba, katika ujenzi wa nchi yetu na kuhakikisha Watanzania wanakuwa wamoja, Rais Samia Suluhu Hassan amekuja na 'R' zipatazo nne ambazo ni Reconciliation (Maridhiano), Resilience (Ustahimilivu), Reform (Mabadiliko) na Rebuiding (Kujenga upya).

Katika kuthibitisha nia hiyo ya Rais, Kinana anasema lengo la mazungumzo hayo ni kutafuta matunda ya pamoja ya maridhiano ya kitaifa ikiwamo amani na utulivu, umoja wa Watanzania na mshikamano wa kitaifa.

Anasema viongozi wa Chadema baada ya mazungumzo ya maridhiano kuanza waliomba wapewe fedha hizo za miaka mitatu walizozigomea swali!

"Wakasema tunadai ruzuku,

Siasa

sisi tangu uchaguzi umekwisha hatujachukua ruzuku. Sasa kwa kuwa tunazungumza na tumeshaanza kuelewana, tulipeni ruzuku yetu ya miaka mitatu," anasema Kinana.

Anasema ingawa kwa kanuni ya ruzuku, mwaka ukipita bila kuchukuliwa haiwezi kusogezwa kwenye mwaka unaofuata, lakini Rais Samia baada ya kushauriana na serikali yake, aliiagiza itafute utaratibu wa kuwalipa ili wapate haki yao.

"Kwa nini hawakuzichukua mwanzoni, ni kwa sababu hawakutambua matokeo. Wakasema mkitupa hizi hela itakuwa mwanzo mzuri wa kutambuana. Tukasema hatuwapi fedha ili mtutambue bali tunawapa kwa sababu tupo kwenye mazungumzo ya kiungwana kwa hiyo wakalipwa Sh bilioni 2.7 ikiwa ni madai yao ya tangu uchaguzi ulipokwisha," aliongeza.

Lakini Kinana anashangaa hakuna kokote ambako mpaka sasa Chadema wameeleza kuwa serikali imewalipa fedha hizo kama ruzuku yao ya tangu Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 ulipomalizika.

Kinana anaona ingekuwa kitendo cha uungwana kwa chama hicho kusema kuwa mazungumzo yanaendelea na kwamba wamelipwa fedha hizo.

"Nadhani ni suala la uungwana tu, kusema mazungumzo haya yalikuwa mazuri kwa kweli tulikwenda vizuri tumeelewana. Tulikuwa na madai yetu yaliyopitwa na wakati lakini watu wamefumba macho, tumelipwa hela zetu," anasema.

**CHADEMA WABINAFSI**

Makamu Mwenyekiti huyo wa CCM anasema mazungumzo yote tangu yameanza mpaka sasa yamejadili hoja nne ambazo zote zimewasilishwa na Chadema. Hata hivyo anasema ni kama chama hicho kinataka kila kitu kinachojadiliwa kiwe ni cha kwao na kuwanyima CCM kuwasilisha hoja zao pia!

Anasema Chadema ndio wamefaidi kwa sababu ajenda zao pekee ndio zimekuwa zikijalidiwa na kutolewa maamuzi lakini upande wa CCM haujanufaika chochote kutokana na kujadili hoja za upande mmoja tu.

Kuhusu suala la Katiba, Kinana anasema kwa upande wao waliona hilo sio jambo la CCM na Chadema bali ni la Watanzania wote, ni la vyama vyote, wasio na vyama na makundi yote.

Lakini anaweka hadharani kwamba jibu la Chadema lilikuwa la ubinafsi wakisema hapa nchini kuna vyama viwili tu, CCM na Chadema na kwamba wakikubaliana wao, wengine watafuata tu mithili ya bendera fuata upepo!

**CHADEMA WAKWAMISHA MAZUNGUMZO**

Kinana anasema kauli na matendo yasiyo ya kiungwana ya Chadema yamekwamisha mazungumzo ya maridhiano baina ya vyama hivyo.

Anasema baada ya serikali kuruhusu mikutano ya hadhara, walikubaliana kuwa kama mtu anataka kukosoa, basi ikosolewe serikali au CCM lakini si mtu binafsi.

Yaani Kinana anamaanisha mtu mwenye dongo lake analotaka kurusha kwenye mkutano wa hadhara aseme, kwa mfano, "Katika hili, serikali imekosea" lakini wao wameendeleza hulka ya kushambulia mtu, "fulani kakosea kwa hatua hii..."

Mkongwe huyo wa siasa anaeleza kusikitishwa na kitendo cha viongozi wa Chadema inapofika sehemu ya kumtaja mkuu wa nchi hawamtaji kwa cheo chake kwa maana ya Rais Samia Suluhu Hassan badala yake wanataja jina tupu, kitendo kinachomshushia heshima na hadhi yake.

Anasema hata baada ya viongozi wa CCM waliokuwa katika mazungumzo walipowaomba kujaribu kumheshimu Rais wa nchi kwa kumtaja kwa cheo chake, hawakutaka kusikia hilo na kuendelea na kejeli zao.

Anasema CCM ingependa kuendelea na mazungumzo lakini itakuwa ngumu kutokana na hali hiyo kwamba jioni kiongozi wake anadhalilishwa na kesho asubuhi wanakutana na kunywa chai pamoja na baadaye dhihaka zinaendelea.

"Sasa tutaendaje kwenye mazungumzo katika hali hiyo. Jana kiongozi wenu kadhalilishwa, asubuhi mnakutana mambo ni yale yale tukafanya hivyo mara ya kwanza, ya pili, ya tatu na ya nne mwisho tukachoka, tukasema hapa tutaonekana watu wa hovyo.

"Yaani tunatukanwa, tunakuja kwenye kikao, tunadhalilishwa tunaendelea na kikao na tunadharauliwa tunaendelea na kikao. Hata siku moja sijasikia neno 'samahani, tutajitahidi haya hayatafanyika tena' kwa lengo la kuimarisha maridhiano, umoja na mshikamano."

Kinana anasema wakati wa mazungumzo yanaendelea aliendа kwa Rais Samia na kumweleza ugumu wa mazungumzo na jinsi jamaa wasivyo waungwana lakini kiongozi huyo wa nchi akamweleza aende nao polepole.

Kinana anaweka wazi kwamba Rais Samia anasikia yote yanayozungumzwa kuhusu yeye lakini Mungu amemjaalia kuwa kiongozi asiye na papara, chuki, kinyongo wala hasira ingawa ana mamlaka na uwezo wa kuchukua hatua kali dhidi ya wanaomkejeli licha ya juhudi zake kubwa za kutaka maridhiano na anayoyafanya katika kuwaletea wananchi maendeleo.

Kinana amekaririwa pia na HabariLeo akisema kitu kingine kilichokwamisha mazungumzo kuwa ni viongozi wa Chadema kutaka kila jambo wanaloleta mezani lipatiwe ufumbuzi hapohapo, wakati kimsingi mazungumzo na serikali siku zote ni mchakato.

Anataja sababu nyingine inayokwamisha mazungumzo hayo kuwa ni matumizi mabaya ya vikao hivyo yaliyokuwa yakifanywa na Chadema kwa sababu kila kikao kwa sehemu kubwa Chadema ndio waliokuwa wakileta manung'uniko, mambo yaliyowasibu au matatizo waliyoyapata ili serikali ione namna ya kuweza kuyatatua.

"Wakaona ni sehemu ya kupatia kila kitu wanachokitaka katika nchi hii."

Kinana anasema viongozi wa Chadema walitaka katika mchakato wa kujadili na kuandaa Katiba mpya suala la serikali tatu lizingatiwe, kitu ambacho kinaenda kinyume na msimamo wa CCM.

**HAWAELEWEKI WANATAKA NINI**

Kinana ambaye aliongoza ujumbe wa CCM katika mazungumzo hayo anasema: "Sasa hivi wamekuja na ajenda nyingine; hali ngumu ya maisha... Kwani wana-CCM hawaguswi na ugumu wa maisha? Rais Samia Suluhu Hassan mwaka jana aliwekeza shilingi bilioni 100 kila mwezi kukabiliana na bei ya mafuta, mbona hili hawalisemi?" Anahoji.

Rais pia ameweka ruzuku kwenye mbolea na mengine lukuki katika kuleta ahueni ya maisha kwa Watanzania lakini Chadema hawasemi au hawaoni!

Kinana amewataka Chadema wawe na msimamo na watambue wanataka nini badala kupinga kila kitu.

"Chadema hawaeleweki wanataka nini. Hapohapo wanaandamana, hapohapo walipeleka watu bungeni kutoa maoni yao, hapohapo wanataka maboresho ya sheria, hapohapo wanaandamana kupinga muswada wa sheria... Yaani, hawaeleweki wanataka nini hasa?"

**MANENO KUNTU**

Lakini maneno haya ya mkongwe huyo wa siasa nchini na ambayo yanahitimisha makala haya yanapaswa kuzingatiwa na kila Mtanzania ikiwemo Chadema yenyewe.

"Niwasihi Watanzania tushikamane, tudumishe amani na umoja, ni kweli yapo matatizo mengi ya kiuchumi, kijamii lakini yanashughulikiwa kwa kadri ya uwezo wa nchi yetu. Tukigeuza kila tatizo ni jambo kubwa linahitaji kushughulikiwa na lisiposhughulikiwa basi ni lazima tusukumane, tupigane, tupambane sio sawa."



Afya

# Faida na hatari kiafya za ulaji wa kuku wa ‘kizungu’



NCHI nyingi za Afrika, wafugaji wengi hutegemea zaidi kuku wa kisasa maarufu kama kuku wa kizungu.

Kuku hawa pia huitwa kuku wa nyama, wamepewa majina hayo kutokana na nyama yake na ukuaji wake wa haraka.

Wamekuwa maarufu kwa sababu huwaingizia wafugaji fedha nyingi katika muda mfupi tofauti na kuku wa kienyeji ambao hujulikana kama kuku wa baiskeli kutokana na kuchukua kukua kwa muda mrefu zaidi.

Katika soko la Afrika, walaji, hasa wale wenye bajeti ndogo, hupendelea kuku wa kisasa kwa sababu huuzwa kwa bei nafuu kuliko kuku wa kienyeji ambao ni ghali zaidi.

Makala hii inaangalia zaidi kuku wa kisasa au wa kizungu kama wanavyofahamika na wengi.

“Kwa sababu unapoweka kuku wa kienyeji au wa asili sokoni, watu huwaona kuwa ni wa gharama sana ingawa ni kuku wenye afya zaidi na wana virutubisho muhimu zaidi kwa mwili,” anasema mmoja wafugaji wa kuku, Eugène Marco, mkazi wa Mbezi Luis, jijini Dar es Salaam.

Hata hivyo, wataalamu wa lishe, hupendekeza ulaji wa nyama nyeupe kwa kuwa wana faida nyingi mwilini.

Wafugaji wa kuku wa kisasa, hupata faida zaidi katika ufugaji wa kuku wa nyama.

“Uzalishaji wao ni wa haraka na wana faida zaidi kuliko kuku wa kienyeji ambao huchukua muda mrefu zaidi na rasilimali,” anaongeza Marco.

Aidha, anadokeza kuwa huchukua siku 21 kwa yai la kuku wa nyama kukomaa na kuwa kifaranga ambacho kitakuwa tayari kuliwa ndani ya miezi mitatu tu.

“Hapa, katika soko la Shekilango, kuku wa kienyeji huuzwa kati ya Sh. 20,000 hadi 30 000 huku wale wa nyama wakigharimu kati ya Sh. 5,500 hadi 6,500.

“Unaweza kuona tofauti kidogo. Ni wazi kwamba tunaweza kumudu kununua tu kile ambacho ni cha bei nafuu, kutokana na matatizo ya sasa ya kifedha,” Rehema Ismail, mama wa nyumbani, anasema.

Hata hivyo, kwa mujibu wa mtaalamu wa lishe na mtaalamu wa usafi na ubora wa chakula, Dk. Matthieu Tobossi, kuku wa kisasa wanafaa kuliwa kwa kiasi, ikizingatiwa kuwa ni sehemu ya viumbe vilivyobadilishwa vinasaba (GMOs).

Hii ndiyo sababu kuu ya ufugaji wa kuku duniani hivi sasa. Kuku hawa lazima wazalishwe haraka na kwa wingi ili kukidhi mahitaji ya nyama yanayoongezeka kila mara.

“Migahawa na hoteli, ndiyo inayowahitaji zaidi. Ni lazima tukidhi mahitaji yao. Kwa hiyo, hatuwezi kutarajia kuku wa kienyeji au wa asili katika kiwango hiki.

Kuku wa nyama hukidhi vyema mahitaji haya. Tunajaribu kupunguza usambazaji wa kemikali kwa kuku hawa kwa njia bora iwezekanavyo,” anasema Levina George, mfugaji wa kuku mkazi wa Kimara jijini Dar es Salaam.

Kuku hawa wanaofugwa kwa ajili ya uzalishaji wa nyama, pia huitwa grill na huwapa walaji virutubisho, kulingana na wataalamu wa lishe. Ni chanzo muhimu cha lishe kwa umma kwa ujumla.

**THAMANI YA LISHE**

Mbali na maonyo hayo kutoka kwa wataalamu wa lishe, mara nyingi yanaonyesha kuwa kuku kwa ujumla, ikiwa ni pamoja na nyama, ina vitamini nyingi na vitu vingine vingi vinavyotoa thamani kubwa ya lishe kwa mwili wa binadamu.

Zaidi ya kemikali zinazodungwa kwenye kuku wa nyama ili kuwafanya wakue na kuliwa haraka, pia wana vitu vya kuvutia kama kuku wengine.

Kuku wa kisasa mara nyingi hulishwa ngano, mahindi, lakini pia protini, vitamini na kufuatiliwa kiafya.

Asidi muhimu za mafuta, pia ni sehemu ya lishe yao ambayo huchangia thamani ya lishe ya nyama yao kwa mwili wa binadamu, kulingana na Dk Tobossi.

Tunaweza kuelewa kuwa kuku huyu ana thamani ya lishe kama nyama nyingine nyeupe.

Seli zote za tishu zilizo hai na protini, ni muhimu kwa utendaji mzuri wa mwili. Kuku wa nyama huwa na protini zinazochangia ukuaji wa misuli. Kwa hiyo, kula kuku ni muhimu kwa misuli, mifupa na homoni, kulingana na wataalamu wa lishe.

Wanasema nyama ya kuku hutoa asidi ya amino ambayo mwili hauwezi kuizalisha. Ni kupitia chakula, hasa kuku, kwamba asidi hizi muhimu za amino hutolewa kwa mwili.

Kutokana na lishe yake, kuku hawa wana vitamini nyingi. Nyama yake hutoa vitamini B3 inayoitwa niasini. Ni vitamini ambayo husaidia kuweka ngozi kuwa na afya. Pia kuna vitamini B6 ambayo inashiriki katika mchakato wa udhibiti na ujenzi wa tishu kutoka kwa protini.

Kuku pia wana vitamini B5 au asidi ya pantothenic, muhimu kwa upyaji wa ngozi na nywele. Pia husaidia utendaji mzuri wa mfumo wa kinga.

Wataalamu wa lishe wanapendekeza ulaji wa nyama ya kuku badala ya ngozi. Gram 100 ya nyama ya kuku, hutoa zaidi ya asilimia 50 ya lishe ya kila siku.

Hizi ni kalori, vitamini na madini ambayo hutolewa kwa mwili. Kuku huitwa chakula cha wajenzi, kulingana na Dk. Tobossi.

“Inapendekezwa kwa watoto, wazee, wajawazito, wanamichezo, wagonjwa n.k. “, anasisitiza.

Lakini jihadhari na kuku wa nyama (kuku wa kisasa, au wa kizungu)

Wafugaji wengi hutumia kemikali na homoni za ukuaji ili kuwa na kiasi kikubwa cha kuku wa nyama kwa muda mfupi sana. Na kwa hiyo matumizi yake ya mara kwa mara, yanaweza kusababisha matatizo ya kiafya, kwa mujibu wa wataalamu wa lishe wanaodai kuwa ni kwa sababu ya kemikali zinazotumika kwa ukuaji wa haraka wa kuku hawa.

“Tuligundua kuwa baadhi ya wafugaji hutumia kupita kiasi dawa za antibiotiki kwa kuku kupita kiasi. Hii husababisha bakteria wa matumbo na straphylococci kuongezeka,” anasema Dk. Tobossi, ambaye anasisitiza kuwa ndiyo chanzo cha magonjwa ya moyo na mishipa na kudhoofika kwa mfumo wa kinga.

“Hii ndiyo sababu kila mara tumeshauri ulaji wa kuku wa nyama kwa kiasi, wakati hakuna kuku wa kienyeji au wa asili,” anasisitiza.

Nyama hii ina mabaki na chembe chembe nyingine za kemikali ambazo ni hatari, hasa kwa moyo. Zaidi ya hayo, kuku wa nyama hulelewa katika mazingira ambayo siyo ya asili kwa ndege hawa, ambayo hupunguza ubora wa nyama yao.

Kwa sababu ya matunzo yao, wana uwezekano wa kuwa sababu ya magonjwa fulani, kwamba watu wanaombwa kupika nyama vizuri kabla ya kula.

Mjasiriamali Haruna Jafary, anaongeza: “Kuna washiriki wa chama chetu ambao hujiingiza katika mazoea ya kuchinja kuku wanapotambua kwamba ni wagonjwa.


Bila kuelewa, huchinja na kupeleka sokoni. Hii ni tabia ambayo tunajaribu kuipiga marufuku.”

Kwa mtaalamu wa lishe, aina hii ya kuku, lazima wachomwe ili kuepusha tatizo la afya ya umma.

Kwa vyovyote wasemavyo watu, chochote kuku ni chakula kizuri ambacho hutoa virutubisho vingi kwa mwili. Lakini lazima tuwe waangalifu tunapotumia kuku wa nyama ambao ingawa pia wana viwango vya lishe, lazima waliwe kwa kiasi kutokana na mazingira wanayofugwa.

***BBC.***

# Maajabu ya samaki Salmon



SAMAKI salmon anatajwa kuwa adimu duniani. Ni samaki anayepatikana pia katika mito mbalimbali wilayani Makete.

Makala hii ya **PETER SOYALA** kutoka Idara ya Maliasili na Mazingira Wilaya ya Makete kama inavyopatikana katika Tovuti ya Halmashauri ya Wilaya hiyo inaeleza zaidi maajabu ya samaki huyu.

**Wataalamu wanatueleza kuwa samaki huyu anaweza kupajua mtoni alipozaliwa kwa kutumia harufu ya maji. Inaelezwa kuwa samaki hawa wanaweza kutofautisha harufu za maji hata kwa kiwango kidogo sana. Samaki huyu pindi anapozaliwa kule mtoni harufu na maji ya eneo alipozaliwa anakuwa na kumbukumbu nayo bila ya kujali amekaa baharini kwa muda gani.**

Salmon ni samaki maarufu sana duniani. Ukiacha minofu mingi aliyonayo, mafuta yake ni mujarabu katika kulinda afya ya mwili dhidi ya maradhi pamoja na kusaidia ukuaji mzuri wa mwili na akili hususan kwa watoto wadogo.

Samaki huyu anapatikana sana kwenye mito iliyopo Amerika ya Kaskazini na wakoloni walipandikiza pia katika mito mbalimbali ya Wilaya ya Makete nchini.

Samaki hawa maarufu wanapatikana kwa wingi sana katika Mto Luvanyina kwa Makete na mito mingine mikubwa.

Miongoni mwa maajabu ya samaki hawa ni safari yao ndefu ya kutembea kutoka mtoni kwenda baharini au ziwani na kurejea tena walipotoka baada ya kukaa muda mrefu wakiwa baharini au ziwani.

Samaki huyu anasifa ya kuishi kwenye maji baridi na maji ya chumvi. Maisha ya samaki hawa yanaanzia pale samaki jike anapotaga mayai maeneo ya juu ya mto ambako kuna maji ya baridi (yasiyo na chumvi). Baada ya kutotolewa, samaki hawa wanakaa mtoni hapo kwa muda kadhaa na baada ya kwisha kukua kiasi cha kuweza kujitafutia chakula wenyewe na kuweza kujilinda hapa wanaanza safari yao ya maajabu sana.

Salmon baada ya kukua na kukomaa anaanza kusogea karibu na bahari au ziwa, na hapa mabadiliko huanza kutokea kwenye mwili wake ili kumfanya aishi kwenye maji ya chumvi.

Baada ya kuweza kuendana na mazingira ya maji ya chumvi na hali ya hewa salmon wanaanza safari yao ya kuelekea baharini ambapo watakaa kwa muda mrefu sana.

Safari ya samaki hawa inaweza kuwa na urefu kuanzia kilomita 1,600 mpaka kilomita 4,000 inategemea aina ya samaki hawa. Inakadiriwa kuwa wakati wa safari yao samaki hawa huweza kutembea kwa umbali wa kilomita sita mpaka saba kwa siku.

Baada ya kizazi hiki kuhamia baharini na kukaa kwa muda wa miaka kadhaa, samaki hawa wanapotaka kutaga na ili kuendeleza kizazi wanarudi kule walipozaliwa, yaani mtoni. Na hapa safari ya kurudi iliyo na maajabu ndipo huanzia.

Itambulike kuwa samaki hawa wanatakiwa kurudi pale walipozaliwa na haijalishi ni muda gani toka waondoke lakini lazima watafika. Pia kwa kuwa maji ya mto yanaelekea baharini na samaki hawa wanarudi mtoni walipozaliwa basi safari yao itakuwa inapingana na maji ya mto. Hivyo itawalazimu kukinzana na nguvu ya maji ya mto na wakati mwingine wanapokutana kwenye maporomoko ya maji wanatakiwa waruke.

Safari hii imejawa uvumilivu kwani kuna wanyama walao samaki huwa wanawasubiria maeneo haya yenye maporomoko pindi wanaporuka wawale. Samaki hawa wanaweza kuruka maporomoko yenye urefu unaokadiriwa kufikia mita tatu. Pia Salmon anaweza kukutana na sehemu ya mto ambayo ina maji kidogo na pamekauka, samaki huyu anaamua kuruka ili ayapate maji ama atasubiria mpaka maji yaingie aendelee na safari yake.

Wataalamu wanatueleza kuwa samaki huyu anaweza kupajua mtoni alipozaliwa kwa kutumia harufu ya maji. Inaelezwa kuwa samaki hawa wanaweza kutofautisha harufu za maji hata kwa kiwango kidogo sana. Samaki huyu pindi anapozaliwa kule mtoni harufu na maji ya eneo alipozaliwa anakuwa na kumbukumbu nayo bila ya kujali amekaa baharini kwa muda gani.

Salmon baada ya safari ndefu na iliyo ngumu anarudi mtoni ambako amezaliwa. Salmon akiwa kwenye safari yake, mwili wake hufanya mabadiliko ambayo yatamfanya aweze kuishi kwenye maji ya baridi. Hii ni tofauti na samaki wengine ambao ukimtoa maji ya baridi papo kwa papo na ukamtia maji ya chumvi hufa. Salmon ana uwezo wa kuishi mazingira yote haya.

Baada ya kuwasili mtoni pale walipozaliwa samaki hawa wanataga mayai na kuyatotoa. Makinda yanapototolewa yanakuwa hayana uwezo wa kujilinda hivyo wanajificha kwenye mawe, baada ya wiki kupita hatimaye samaki hawa wanaweza kujitafutia chakula wenyewe safari hii huanza tena. Na haya ndio maisha ya samaki huyu salmon.

Nani kamfundisha samaki huyu kujua mazingira na maeneo alikozaliwa, na kuweza kurudi bila ya kukosea. Kwa nini samaki huyu anatembea safari hii iliyo na ugumu na uvumilivu?

Salmon ni samaki ambaye anatupatia mafunzo mengi sana. Kwa mfano, siku zote hutakiwa kukabiliana na changamoto kwani kukimbia siyo njia sahihi ya kutatua tatua tatizo. Salmon anaenelea na safari yake bila ya kujali nguvu ya maji ya mto kuwa itamrudisha baharini, hivyo anaendelea kukabiliana na magumu hayo.

Kwa mujibu wa BBC kuna faida tano za kula samaki wenye mafuta akiwemo salmon.

**I.Huzuia ugonjwa wa moyo**

Tafiti nyingi zimeonesha kuwa samaki huyu ana asidi ya mafuta ya omega-3 inaweza kusaidia watu kupunguza cholesterol na shinikizo la damu, na hivyo kupunguza hatari ya ugonjwa wa moyo.

**II. Kulinda seli za neva dhidi ya uharibifu, kuzorota, au kuharibika**

Asidi ya mafuta ya Omega-3, haswa DHA, ni muhimu kwa ukuaji bora wa ubongo na utendakazi wa ubongo na husababisha kuzuia magonjwa ya neurodegenerative, pamoja na ugonjwa wa kupoteza kumbukumbu.

**III. Ni nzuri kwa viungo vya mwili**

Asidi ya mafuta ya Omega-3 kwa asili huzuia mzio mwilini, tafiti kadhaa zinaonesha kuwa hulinda viungo vya mwili, na zinaweza kusaidia kuzuia ugonjwa wa baridi yabisi.

**IV. Inasaidia afya ya akili**

Utafiti muhimu unaonesha kuwa asidi ya mafuta ya Omega-3 ina athari ya faida kwa afya ya akili, pamoja na wasiwasi na unyongovu.

**V. Humsaidia mtu aliye katika hatari ya kupata saratani**

Tafiti nyingi zimeonesha kuwa asidi ya mafuta ya omega-3 inahusishwa na kupunguza hatari ya saratani fulani, pamoja na saratani ya utumbo na matiti.

Inapendekezwa kula samaki wa mafuta angalau mara mbili kwa wiki.

**Makala hii imeandaliwa na mwandishi Godfrey Sanga**



# Kurunzi

Na Dk. Reubeni Lumbagala | 0620 800 462

# Rushwa; tuzibe nyufa sasa tuepuke kujenga ukuta



“MSIDHANI katika awamu ya kwanza hapakuwa na rushwa. Rushwa ilikuwepo, lakini tulikuwa wakali! Tulitaka viongozi wetu watambue hilo, hatukufanya mchezo na rushwa hata kidogo! Na kiongozi akishathibitika amepokea rushwa, kazi hatukumuachia hakimu peke yake, Ehe viongozi wetu mnakula rushwa? (kicheko)! Akishathibitika amekula rushwa, alihukumiwa kifungo kisichopungua miaka miwili jela, viboko ishirini na vinne; kumi na viwili siku anaingia gerezani na kumi na viwili siku anatoka, akamwoneshe mkewe (kicheko)!

“Wote wawili tuliwapa msukosuko, aliyetoa na aliyepokea, Wazanaki wanasema; ‘Bose manzi ga nyanja’ (wote wanasombwa na maji). Kwa hiyo hatukuwa na mzaha na rushwa hata kidogo.”

Hayo ni maneno ya Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere wakati akimzungumzia tatizo la rushwa ambalo imenipendeza kulizingumzia leo katika safu hii.

Moja ya tafsiri ya neno ‘rushwa’ ni hali ya kutoa fedha au kitu ili kupata upendeleo. Kwa lugha nyingine ni hali ya kupata haki ambayo si yako na mara nyingi yule mwenye haki sawia anaikosa. Ndiyo maana Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere alipenda kusisitiza kwamba rushwa ni adui wa haki.

Rushwa, kama kiini au sehemu ya ufisadi pia ina maana ya matumizi mabaya ya ofisi kwa maslahi binafsi. Yaani rushwa huwezi kuitenga na ‘umimi’ au ubinfasi. Hali ya kujali maslahi yako na tumbo lako lakini maslahi ya mwingine, wengine, jamii au hata nchi yako hayakuhusu!

Kwa tafsiri hizo, rushwa ni tatizo hatari la kijamii. Kuna watu wamepoteza haki, wamepoteza mali wamefungwa au kukosa maendeleo kwa ajili ya rushwa.

Rushwa kubwakubwa zimesababisha kundi au kigenge cha watu wachache kuneemeka, wakasomesha watoto wao Ulaya huku jamii kubwa unayowazunguka ikitopea katika umaskini wa kutupwa.

Kutoka na athari hasi za rushwa, takribani kila nchi inafanya jitihada zake katika kupunguza au kukomesha rushwa kabisa.

Kwa mfano, baada ya Marekani kuiondoa Uganda katika Mpango wa Ukuzaji wa Fursa za Biashara Afrika (AGOA) unaoiwezesha nchi hiyo kuingiza bidhaa bila vikwazo vya kiushuru Marekani, Rais wa Uganda, Yoweri Museveni amesema: “Kama Waganda tutashikamana na kudhibiti rushwa, hatua hii ya kunyimwa fursa za Agoa haitatukisa.”

Kwa hiyo Museveni analia rushwa kwamba unaweza kuyumbusha ustawi wa watu wake katika kipindi hiki cha kukosa fursa za Agoa huku akihimiza mshikamano.

Tanzania si kisiwa, rushwa inaikabili pia nchi yetu na ndiyo maana juhudi mbalimbali zinafanyika kuhakikisha tunapunguza rushwa kwa kiwango kikubwa au kuimaliza kabisa.

Ipo methali isemayo “Usipoziba ufa utajenga ukuta.” Methali hii inatuhimiza kuwa tusiporekebisha jambo linapokuwa dogo, baadaye tatizo litakuwa kubwa sana na madhara yake yatakuwa makubwa zaidi.

Pia methali hii inamaanisha ukidharau jambo dogo, linaweza kuongezeka na kuwa kubwa zaidi au usipozuia mambo madogo madogo yatakuwa mazito baadaye. Ndio maana waswahili pia wanasema; mdharau mwiba, mguu huota tende.

Kutokana na uwepo wa rushwa katika maeneo mbalimbali kama vile mahakamani, hospitalini, ofisi za umma, shuleni/vyuoni na maeneo mengine, ni muhimu kuweka jitihada kubwa katika kuzuia (prevention) kuliko kupambana (combating) kwani gharama za mapambano ni kubwa sana kuliko za kuzuia.

Vita ya rushwa ni jukumu la kila mwananchi na si serikali peke yake. Ndiyo maana ni muhimu mno kuunganisha nguvu ya pamoja kupitia serikali na taasisi zake kama vile Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), asasi za kiraia na wananchi, ili kupiga hatua kubwa katika vita ya rushwa.

Desemba 4, mwaka 2023, akiwa kwenye kongamano la jukwaa la kitaifa la wadau dhidi ya rushwa ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Wiki ya Maadili na Haki za Binadamu nchini, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora, George Simbachawene alizitaka taasisi zinazohusika katika kusimamia utawala bora nchini, kujikita zaidi kuzuia rushwa badala ya kupambana nayo.

Simbachawene alikemea hali iliyopo sasa ya kupambana na rushwa kwenye miradi ya maendeleo badala ya kuzuia rushwa isitokee ili kupata thamani ya fedha (value for money) kwenye miradi hiyo ili kuleta tija kwenye maisha ya wananchi.

“Wakati mwingine tunaweka nguvu kubwa na raslimali nyingi katika katika kupambana na rushwa wakati ambapo matokeo ya rushwa yanakuwa tayari yameshatokea na kuleta madhara kwa serikali badala yake tulipaswa kutumia nguvu hiyo hiyo katika kuzuia rushwa isiweze kutokea,” anasema Simbachawene.

Vilevile, Simbachawene alirejea kwenye tafiti mbalimbali zilizofanywa nchini kuhusu hali ya utawala bora nchini ambapo tafiti zimebaini kuwa rushwa ni moja ya changamoto katika ufikiwaji wa lengo la serikali la kuhakikisha kuwa wananchi wanapata maendeleo katika sekta kama vile maji, afya, elimu na miundombinu.“

“Niwahakikishieni serikali yetu haitaacha kukabiliana na vitendo vya rushwa na kupambana inapobidi kwa kuwa zipo njia mbalimbali za kuzuia rushwa isiweze kutokea mojawapo ni hii ya kujadili pamoja mbinu za kuboresha zaidi usimamizi wa miradi ya maendeleo,” anasema Simbachawene.

Kutokana na tafiti kuonesha rushwa inaathiri ufikiwaji wa maendeleo ya wananchi, hivyo basi ni muhimu kuzuia rushwa ili kuepuka kadhia hii ambayo inaathiri maisha ya wananchi kutokana na miradi kutekelezwa chini ya kiwango au wananchi kukosa kabisa miradi ya maendeleo ambaye kama ingetekelezwa ipasavyo, ingeweza kuboresha hali za maisha za wananchi na kuchochea kasi kubwa ya maendeleo kwa ustawi wa wananchi na nchi kwa ujumla.

Ni muda mwafaka sasa kuhakikisha kuwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo, kanuni na sheria zote zinazingatiwa ili kuondoa mianya ya rushwa.

Mathalani, upatikanaji wa mzabuni wa kutekeleza miradi ya maendelo, apatikane kwa uwazi na akidhi vigezo vyote. Vilevile, hata baada ya kushinda zabuni hiyo, mzabuni afuate sheria za manunuzi kikamilifu katika utekelezaji wa mradi ili mradi uakisi thamani ya fedha na wananchi wafurahie mradi huo.

Kama hatutaziba nyufa za kutenda haki kwa wazabuni wanaotekeleza miradi ya maendeleo na kufuatilia ubora wa kazi, ni dhahiri watapatikana wazabuni wasiokidhi vigezo na hivyo kutekeleza miradi chini ya kiwango, ambapo itakuwa ni upotevu wa fedha za umma na kuwakosesha wananchi miradi yenye ubora.

Ni lazima ieleweke kuwa gharama ya kuzuia rushwa ni ndogo kuliko ya kupambana nayo. Uchaguzi ni wetu, kutumia gharama ndogo kuzuia au kutumia gharama kubwa katika mapambano.

Nchi yetu bado ni maskini, bila kuzuia rushwa, wananchi wa chini ambao ni wengi watapata shida kupata haki zao. Kila mwananchi awe wa kipato cha juu, kati au chini anapaswa afurahie kuishi Tanzania kwa kupata haki bila rushwa. Usipoziba ufa utajenga ukuta. Tusifike huko kwenye mapambano ya rushwa, tunayo nafasi ya kuziba nyufa sasa na kujenga mwelekeo mzuri wa nchi yetu kwa maendeleo endelevu.

Mtoa rushwa na mpokea ‘wote wasombwe na maji’ mara moja.



Paul Mng'ong'o

KLINIKI YA FIKRA

Simu: 0676055444 Email: mngongopaul@yahoo.com

# Misumari ya mahusiano - 5

WIKI iliyopita tuliendelea na somo hili lenye makusudi ya kuimarisha na kuamua kwa dhati mahusiano yetu. Mambo haya unaweza kuyachukulia kirahisi au kutoyapa uzito lakini ukiyazingatia na kuamua kwa dhati kuyatekeleza, huleta uimara wa mahusiano, amani na kuwajengea furaha. Karibu tuendelee safu hii sehemu ya tano kwa faida yako na ustawi wa jamii yetu.

**20. HAKI (JUST)**

Kila mtu anataka mwenzi anayeweza kumwamini, awe ni mwadilifu na mwenye msimamo kwenye haki na hekima wakati panapotokea nyakati ngumu na kuhitaji maamuzi magumu.

Kuna muda utajikuta kwenye nyakati ngumu kwenye mahusiano yenu. Kwa mfano, mama yako na mwenzi wako wanaweza kuingia katika hali ya kutoelewani au dada yako na mwenzi wako hawakubaliani. Hali hizi huibuka kwenye maisha.

Hapa ndipo mwenzi wako anahitaji kukuona ukitumia akili kubwa, kuangalia ilipo haki na kuonesha umakini mkubwa.

Ingawa si kila mara lakini mara kwa mara migogoro hii huwatokea wanawake. Hapa sasa mke huyohuyo anahitaji kuona uwezo wako wa kurekebisha hali kwa hekima bila kuiacha haki kupotea.

**21. USAFI (KEMPT)**

Watu wengi wanapenda wenza wasafi. Hili ni hitaji kubwa zaidi la wanaume. Mwanaume anahitaji mwanamke awe msafi. Hata kama mwanaume mwenyewe si msafi sana, lakini atathamini mwanamke msafi. Hii haimaanishi kwamba mwanaume anatakiwa kuwa mchafu lakini usafi wa mwanamke huwa muhimu sana.

Kwa hivyo, weka mazingira mazuri, hakikisha unakuwa msafi wa maeneo yote nyakati zote na kakikisha unanukia vizuri na unaonekana mwadilifu, nadhifu na wa kisasa.

**22. VITENDO VYA FADHILA (KIND GESTURES)**

Kila mtu anaweza kufanya kitendo cha fadhila. Mara nyingi hata si mambo makubwa. Ni vitendo vidogo ambavyo kwenye fikra vina tafsiri ya fadhila. Mfano shukrani, tabasamu, mwitikio, furaha, kuomba msamaha, ishara za unyenyekevu kama kina dada wana ishara ya kupiga magoti kwa baadhi ya makabila.

Kwa wanaume nao huwa na ishara za heshima na adabu kama kuvua kofia wakati wa kusalimia kuonesha nidhamu, hekima, nk.

Mfano mwingine kwa jamii zetu za kiafrika ni kama mwanaume kumnyooshea nguo mke wake, anamuona mke wake kachoka anamzuia asipike akaagiza chakula kizuri au akapika, kutoa zawadi, mwanaume kuosha gari ya mke wake au mtu kuwa na maneno ya staha kama vile "tafadhali" na mambo mengi yanayofanana na hayo.

Mambo haya yanahitajiwa na wenzi wote lakini mwanamke anayathamini zaidi endapo atafanyiwa na mume wake.

**23. UAMINIFU NA UFUASI (LOYALTY)**

Pamoja na umuhimu wa jambo hili pande zote za mahusiano, jambo hili ni hitaji kubwa kwa mwanaume. Mumeo anahitaji kujua kwamba unamuunga mkono wakati wote na utakuwa nyuma yake daima hata wakati anapitia nyakati ngumu.

Ni muhimu usimame naye akipitia nyakati nzuri na mbaya, si tu kama mtazamaji, bali ukishiriki kikamilifu kupigana kwa ajili yake na pamoja naye.

Wanaume hawapendi kuishi na mtu mkosoaji ambaye mara nyingi kazi yake ni kukosoa na kulalamika. Hivi vyote viwili (kukosoa na kulalamika vina sura ya kutoridhika, kutofurahishwa au kutopenda).

Ni vizuri wakati wote ukahakikisha unaonesha sura ya kumuunga mkono na kuwa nyuma yake huku ukitafuta busara ya kumsaidia maeneo ambayo unahisi hafanyi sawasawa. Ndiyo maana wanawake hawatakiwi kuwa "direct" badala yake wanatakiwa kuwa "indirect".

Mpe mawazo kwa njia ya kumuuliza kana kwamba unataka mwongozo wake lakini swali ulilompa unajua wazi ni swali elekezi.

**24. UONGOZI (LEADERSHIP)**

Kuwa na kiongozi mzuri kama mume ni moja ya zawadi kubwa ambazo mwanamke yeyote anatamani kuwa nayo. Kiongozi hutoa, hulinda na husimamia. Kiongozi (mume) mzuri kwa kadiri awezavyo atamlea mke wake mpaka awe bora kabisa.

Hili litawezana tu endapo mke hatakuwa mtu wa kujisimamia, kujitawala mwenyewe, mkaidi na yeye kutaka kuongoza na kufundisha.

Mke mtulivu na miungwana atatoa nafasi ya uongozi kwa mume wake na hapo anatarajia mume awe mwenye hekima, busara na roho ya uongozi yenye kufundisha ndani yake.

Mfano, mwalimu mmoja wa kike alisema maneno haya: "Nilipokutana na mume wangu, nilikuwa na vipawa na uwezo mwingi ndani yangu ambao haukuwa ukitumika. Lakini mpaka mume wangu alipoanza kusukuma, kulea, kuelekeza na kunionesha kwamba naweza kuwa bora zaidi, ndipo nilipoanza safari kuyaelekea mafanikio. Nisingeweza kufikia hata nusu ya mafanikio yangu ya leo bila uongozi na jitihada zake."

**25. TAAHADILI (MEEK)**

Hii maana yake ni mtu kuwa tayari kujifunza na mwenye kukubali kubadilika. Hili linabeba maana halisi ya utii na unyenyekevu. Mwanamume anataka mke wake aweze kufundishika, kubadilika, na kuwa wazi kwa mabadiliko. Kamwe mwanamke usiwe na kiburi cha kumwomba mumeo msaada pale unapokuwa hujui la kufanya tu.

**Wework Consult - Your Partner in Growth.**

**Itaendelea wiki ijayo...**





**Na Hamisi Kibari**

Mtanzani wa kwanza kushinda Tuzo ya Taifa ya Mwalimu Nyerere ya Uandishi Bunifu

# Niko tayari kwa kifo - 18

**Kutooneka kwa Chris na mkewe kunaleta wasiwasi kwa dada yake, Mwalimu Misango kufikiria kutoa picha kwenye magazeti. Katika hatua nyingine jirani wa Chris alipokuwa akiishi na mkewe anamjulisha Mwalimu Misango wasiwasi walio nao kwamba hawaamini kama mke wa Chris, Mama Kenny, ni mzima kwani toka wasikie Chris akimpiga vibaya hawajamtia machoni. Jirani huyo, Maua anamweleza Mwalimu Misango kitu kingine cha kushangaza, kwamba Mama Kenny amekuwa akijitokeza mtaani kwao, tena mchana kweupe kama mzimu. Katika hatua nyingine Chris akiwa amevaa kofia pana na miwani myeusi anaonekana akimwinda Joyce, msichana mrembo aliyemfilisi kisha kumkataa. Nia yake si njema... Nini mwisho wa mkasa huu? Endelea.**



Kuna wazo lilimjia la kumvamia yule bwana aliyemzidi kete lakini akasita. Kama kuna mtu alikuwa akimchukia zaidi duniani ni mwanaume huyo aliyemchukua mwanamke aliyekuwa akimpenda kupindukia.

Alimwombea kila baya. Alitamani kusikia usiku huo kapinduka na gari lake na kufariki dunia. Akamwona akiwasha gari na kuondoka.

Chris aliona kosa alilofanya mwanaume huyo. Alitakiwa kuhakikisha Joyce anaingia ndani na ndipo aondoke. Lakini kwa hali ilivyo wawili hawa hawakutarajia hatari yoyote katika eneo hilo tulivu hata kama muda ulikuwa umeenda sana. Saa saba kasorobo usiku. Kama ni tishio lake yeye Chris, bila shaka walijua wamesharipoti polisi ingawa hawakuwa na uhakika kama keshakamatwa ama la.

Hata yeye wakati akija kufanya mawindo hayo alikuwa anawaza namna ambavyo angefanikiwa kuingia ndani au kumfanya Joyce atoke nje lakini sasa aliona kazi yake ya kumvamia kabla hajaingia ndani ni nyepesi.

Wapenzi hao wawili hawakujua kwamba mwanaume huyo aliyekuwa sasa akitembea kwa kujifichaficha akivaa kofia pana, miwani myeusi na bandeji kwenye pua, muda mwingi alikuwa bado akifuatilia nyendo zao. Ilikuwa si rahisi kumjua hata kama wangekutana naye. Kwa mfano usiku huo aliwapitia jirani yao wakiwa baa lakini hawakumtambua.

Joyce ambaye muda wote alisimama akimpungia mkono mpenzi wake wa sasa, alishusha mkono uliokuwa unapunga hewani baada ya gari kuondoka na sasa akageuka kujongea nyumba iliyokuwa imesimama mbele yake. Ilikuwa ni nyumba nzuri ndogo iliyo katika eneo ambalo ndio kwanza linajengwa nyumba nyingi za kisasa maarufu kama Makokora. Joyce ambaye ilikuwa ni siku ya tatu kutoka 'viwanja' baada ya varangati alilolifanya yeye Chris na kusababisha alazwe hospitali na kushonwa kichwani, hata gizani alionekana afya yake haijaimarika.

Lakini Chris alimjua kwamba ni mwanamke ambaye ilikuwa ni nadra kulala bila kunywa pombe ama kukaa angalau hata saa sehemu za starehe.

Alipiga hatua kujongea mlango wa kuingilia kwenye nyumba aliyokuwa akiishi akiyumbayumba, na bila shaka pombe nazo zilichangia hali ile. Kichwani alifikiria kutafuta msichana wa kazi awe akimfungulia mlango na kumsaidia mambo mengine kama kufanya usafi wa nyumba na wakati mwingine kumwandalia kifungua kinywa. Wakati Joyce akifungua pochi kutoa ufunguo ili kufungua mlango wa kuingilia, alishituka kusikia kishindo cha mtu kikitokea nyuma yake.

Alijikuta akitetemeka baada ya kugundua hatari iliyokuwa mbele yake.

Alichomoa simu haraka kumpigia simu mpenzi wake baada ya kuhisi haikuwa rahisi kufungua mlango harakaharaka na kuingia kabla ya mwanaume aliyekuwa akimjua kwa kasi hajamwahi. Alihisi ni mwizi au jambazi.

> **Ndio. Niliua mke wangu na leo nimeua. Ninastahili kufa... Lakini kwa nini nisimuue na yule jamaa aliyemrubuni Joyce kwanza kabla na mimi sijachukua uhai wangu...**

"Hallow baby, hatari rudirudi..." Kabla mpenzi wake hajajibu, Chris alikuwa tayari ameshafika na kumtakua ile simu na kisha kuitupa. Kama umeme, Chris almkwida na kumziba pua kwa kitambaa chenye dawa ya kulevya.

Usicheze na kifo! Mwanamke huyo baada ya kuhisi hatari, alijitutumua kutaka kujiondoa kwenye kabali ya Chris bila mafanikio. Pombe zilimruka mwanamke huyo na kujaribu kupiga kelele lakini kutokana na kabali ya Chris sauti yake haikufika kokote.

Baada ya kuhakikisha kwamba ameanza kupoteza fahamu, Chris alimbeba juu juu kuelekea kwenye eneo la vichaka, si mbali sana kutoka nyumba hiyo mpya.

Ni eneo ambalo alilizuru mara mbili alilifanyia uchunguzi.

***

Chris akiwa amevaa kofia pana linaloziba uso wake, aliketi kwenye msingi wa nyumba ya dada yake, jirani na taa ya iliyokuwa inawaka usiku kucha. Nguo zake zilikiwa zimerukiwa na damu. Aliangalia huku na kule hakuona mtu. Mkononi alikuwa ameshikilia kipande cha gazeti alichokiokota eneo hilo. Alichomoa karatasi mbili ndefu ambazo alizitayarisha mapema pamoja kalamu. Kabla ya kuandika alowaza kidogo. Akajisemea."Nilizaliwa siku moja. Na nitakufa siku moja. Lazima leo nimfuate mke wangu kipenzi, Tausi. Ama kwa hakika mshahara wa dhambi ni mauti. Ninastahili kufa... Ndio. Niliua mke wangu na leo nimeua. Ninastahili kufa... Lakini kwa nini nisimuue na yule jamaa aliyemrubuni Joyce kwanza kabla na mimi sijachukua uhai wangu... Hapana. Hana makosa."Chris aliinama. Akaanza kuandika waraka ambao ulionekana ni mrefu. Baada ya kuandika waraka huo, akaufutika kwenye mfuko wa shati aliokuwa amevaa na kuelekea kwenye mwembe ulio pembeni tu mwa dirisha alilokuwa analolala dada yake, Mama Kessy maarufu pia kama Mwalimu Misango.Ndio, Chris aliamini ni nyumba hiyo, kwa dada yake alikoanzia maisha kwa maana ya biashara hadi akaanza kuwa mtu maarufu na ni mahala palipomfaa kumalizia maisha yake hapa duniani. Aliona hana namna ya kuishi. Asipojitundika, atakamatwa na polisi na kuteseka kwa muda mrefu gerezani. Hakuona sababu ya kuwa na mateso mengi kiasi hicho badala ya kukatisha uhai wake mara moja.

Uwezo wake wa kufikiri ulikuwa umegota. Alijiona ni mpweke asiye na kitu na uwezo tena wa kuwasaidia na kiwasomesha watoto wake.

"Ngoja tu wabaki yatima. Ninashukuru kuzaliwa na dada mzuri, muungwana na mwenye maono. Atawalea."

Mama Kessy na mumewe wakiwa wamelala fofofo, ghafla walisikia kishindo kikubwa kutoka nje. Mama Kessy alishtuka, akasikiliza kwa muda roho ikimwenda mbio kisha akamwamsha mumewe.Mumewe, Baba Kessy aliamka. Naye alikuwa kama akiota ndiyo ya kushindo. Mkewe alimweleza kuwa amesikia kishindo kikubwa si mbali sana na lilipodirisha lao. Mumewe ambaye naye alisikia kishindo hicho kama mtu anayeota alichukua tochi. Alichukua simu yake, akaiwasha kutazama saa."We unawasha simu. Acha. Wanaweza wakawa ni majambazi wanatuchungulia. Watahisi unawapigia simu polisi," alisema Mwalimu Misango akinong'ona huku wasiwasi ukizidi kumpanda.

Walisikiliza kwa makini nje lakini wakaona ukimya ukitawala ingawa walihisi michakato kwenye nyumba jirani. Bila shaka nao walisikia kishindo .

Baba Kessy, akiwa ameshika panga aliamua kutoka nje. Sasa aliona umuhimu wa kumiliki bastola kwa sababu kwa nafasi yake alipaswa kuwa nayo. Lakini akaamini kwa wakati huo, panga lingeweza kumfaa kama kuna hatari yoyote.

*Itandelea*

# Watu 10 wauawa wakiwa kituo cha polisi

**ISLAMABAD, Pakistan**

TAKRIBAN maafisa 10 wameuawa katika shambulio la saa moja kwenye kituo cha polisi nchini Pakistan.

Maafisa hao walipoteza maisha baada ya zaidi ya wanamgambo 30 kufanya shambulizi hilo mapema juzi Jumatatu.

Wengine wanne walijeruhiwa katika mapigano hayo yaliyodumu kwa saa mbili na nusu, Mkuu wa Polisi wa Jimbo la Khyber Pakhtunkhwa, aliliambia Shirika la Habari la AFP.

Haijabainika ni nani alihusika na shambulio hilo au ikiwa linahusiana na uchaguzi uliofanyika Alhamisi iliyopita.

Kumekuwa na ongezeko la ghasia katika wiki chache zilizopita ikiwa ni pamoja na mgombea ubunge wa Kitaifa, kuuawa kwa kupigwa risasi katika sehemu nyingine ya Khyber Pakhtunkhwa Jumatano iliyopita.

Hata hivyo, Khyber Pakhtunkhwa pia ina historia ndefu ya mashambulizi dhidi ya shabaha za serikali na usalama pamoja na raia na kundi la Taliban la Pakistan, Islamic State na makundi mengine ya wanamgambo.

Kulingana na Akhtar, Hayat Gandapur, Mkuu wa Polisi wa eneo hilo, mashambulizi hayo yalianzishwa saa 3:00 kwa saa za huko kwanza kwa milio ya risasi ikifuatiwa na magurunet i.

Wanamgambo hao walishambulia kutoka pande tatu tofauti na kwa muda mfupi, walikuwa na udhibiti wa kituo cha polisi, aliongeza. BBC.

> **Hayat Gandapur, Mkuu wa Polisi wa eneo hilo, mashambulizi hayo yalianzishwa saa 3:00 kwa saa za huko kwanza kwa milio ya risasi.**

# Mfalme Charles agunduliwa kuwa na saratani

**LONDON, Uingereza**

MFALME Charles wa Uingereza, amegunduliwa kuwa na saratani, Kasri la Buckingham limetangaza.

Saratani hiyo si ya tezi dume, lakini imegunduliwa hivi karibuni wakati akipatiwa matibabu ya uvimbe katika tezi dume.

Hata hivyo, Kasri la Buckingham halijaweka wazi aina ya saratani ambayo Mfalme Charles aliyogunduliwa kuwa nayo, lakini kwa mujibu wa taarifa kutoka kwenye kasri hilo, tayari Mfalme alianza matibabu ya kawaida tangu juzi Jumatatu.

Kasri la Buckingham lilisema kwamba Mfalme Charles anasalia na mtazamo chanya juu ya matibabu yake na anatazamia kurejea kutekeleza kazi kamili ya umma haraka iwezekanavyo.

Ataahirisha shughuli zake za umma na inatarajiwa kwamba wanafamilia wengine wakuu wa familia ya Kifalme, watamsaidia shughuli zake za umma wakati wa matibabu yake.

Hakuna maelezo zaidi yaliyotolewa juu ya hatua ya saratani au matibabu atakayopewa.

Ingawa atasitisha hafla zake za umma, Mfalme, mwenye umri wa



miaka 75, ataendelea na jukumu lake la kikatiba kama Mkuu wa Nchi.

Alionekana kwenye ibada ya kanisa huko Sandringham Jumapili iliyopita ambapo alipungia mkono umati.

Alifanyiwa upasuaji wa tezi dume katika hospitali ya kibinafsi ya London zaidi ya wiki moja iliyopita.

Mfalme Charles alikuwa amechagua kujitokeza hadharani kuhusu matibabu yake ya tezi dume, kwa lengo la kuwahimiza wanaume zaidi kupata uchunguzi wa kibofu, ilisema kasri wakati huo.

Alisemekana kuwa alifurahishwa na kuongeza ufahamu kuhusu suala hilo na tovuti ya NHS ikiripoti kuongezeka kwa masuala kuhusu hali ya tezi dume.

Kwa aina nyingi za saratani, nafasi ya kuipata huongezeka kadiri umri unavyoongezeka.

Takwimu za Uingereza zinaonyesha kwa wastani kila mwaka, zaidi ya theluthi (asilimia 36) ya kesi mpya za Saratani, zilikuwa kwa watu wenye umri wa miaka 75 na zaidi.

Waziri Mkuu, Rishi Sunak, amemtakia Mfalme Charles afueni kamili na ya haraka, Kiongozi wa chama Kikuu cha upinzani cha Labour, Sir Keir Starmer, pia amemtakia kheri Mfalme Charles.

Mwandishi wa habari za Familia ya Ufalme Pentagon ilisema wanajeshi watatu waliouawa Jumapili asubuhi walitoka katika kitengo cha wanajeshi wa akiba kilichopo Fort Moore, katika Jimbo la Georgia.

Luteni Jenerali Jody Daniels, Mkuu wa Hifadhi ya Jeshi na Mkuu wa Kamandi ya Jeshi la Akiba ya Marekani, alitoa pongezi kwa wanajeshi waliouawa.

"Kwa niaba ya Jeshi la Akiba, ninashiriki katika majonzi waliyonayo marafiki, familia na wapendwa wao. Utumishi na kujitolea kwao, havitasahaulika na tumejitolea kusaidia wale walioachwa nyuma kutokana na mkasa huu," alisema Jenerali Daniels.

Shambulio hilo la ndege zisizo na rubani lilifanyika Rukban Kaskazini-Mashariki mwa Jordan, karibu na mpaka wa Syria. Kituo hicho kilitajwa baadaye na maafisa wa Marekani kama Tower 22.

BBC.

# Watu 28 wauawa shambulizi mji wa Ukraine

**KYIV, Ukraine**

URUSI imesema takriban watu 28 wameuawa katika shambulio lililotokea kwenye duka la mikate katika mji wa Lysychansk, Mashariki mwa Ukraine unaokaliwa na Urusi.

Jengo hilo ambalo pia lilikuwa na mgahawa unaoitwa Adriatic, lilipigwa Jumamosi iliyopita.

Maafisa wa Urusi walisema wanajeshi, wanawake na mtoto, waliuawa katika shambulio hilo.

Utawala wa Urusi ulisema silaha zilizotolewa na nchi za Magharibi, zilitumika katika shambulio hilo ambalo imeliita kuwa ni kitendo cha kigaidi cha Ukraine.

Kyiv haijatoa maoni yake, lakini wanablogu wa kijeshi wa Ukraine, wamedai washirika na maafisa wa Urusi, walikuwa kwenye jengo hilo wakati huo.

Juzi Jumatatu, Mkuu wa Jamhuri ya Watu wa Luhansk (LNR) iliyounganishwa na Urusi, alisema kuwa shambulizi hilo lilimuua Waziri wa Hali ya Dharura, Alexey Poteleshchenko, ambaye alikuwa akisherehekea siku yake ya kuzaliwa kwenye mgahawa uliopigwa.

Msemaji wa Wizara ya Mambo ya Nje ya Urusi, Maria Zakharova, alisema Jeshi la Ukraine lililenga duka la mikate kwa makusudi, wakijua kwamba wenyeji kwa kawaida huja huko siku za Jumamosi kununua mikate na mboga, ikiwa ni pamoja na wazee na familia zilizo na watoto.

Hakuna idadi ya vifo au madai yoyote ya Urusi au Ukraine, iliyothibitishwa na BBC.



# Shambulio la ndege zisizo na rubani laua wapiganaji sita

**WASHINGTON, Marekani**

SHAMBULIO la ndege zisizo na rubani katika kambi kubwa zaidi ya kijeshi ya Marekani, limewaua takriban wapiganaji sita kutoka kwa wanamgambo washirika wanaoongozwa na Wakurdi.

Jeshi la Kidemokrasia la Syria (SDF) chombo cha angani kisichokuwa na rubani (UAV) kilichorushwa kutoka eneo linalodhibitiwa na Serikali ya Syria, liligonga chuo chake cha makomando katika eneo la mafuta la al-Omar katika Mkoa wa Mashariki.

Kundi la SDF ambalo lilisaidia muungano unaoongozwa na Marekani kushinda kundi la Islamic State Mashariki mwa Syria, liliongeza kuwa uchunguzi wa awali uligundua kuwa wanamgambo wanaoungwa mkono na Iran, ndiyo waliohusika na kitendo cha kigaidi.

Shirika la Uangalizi wa Haki za Kibinadamu la Syria (SOHR)



lenye makao yake makuu nchini Uingereza, limeripoti kuwa makomando saba wa SDF, waliuawa na 18 kujeruhiwa katika shambulio lililotajwa kuwa ni la 108 la wanamgambo kwenye kambi za Marekani nchini humo tangu katikati ya Oktoba, mwaka jana.

Kundi la Islamic Resistance la Iraq, kundi chini ya mwavuli wa wanamgambo wa Iraq wanaoungwa mkono na Iran, lilidai shambulio la ndege isiyo na rubani Jumapili iliyopita dhidi ya kituo kinachokaliwa na Marekani katika eneo la mafuta la al-Omar katika taarifa iliyoripotiwa na vyombo vya habari vya Iraq.

Pia ilidai shambulizi la ndege zisizo na rubani kwenye kambi ya 22 ya Marekani upande wa Jordan kwenye mpaka wa Syria Januari 28, mwaka huu ambalo liliua wanajeshi watatu wa Marekani na kusababisha Marekani kufanya mashambulizi ya anga dhidi ya vituo vya Jeshi la Iran na wanamgambo wanaoungwa mkono Iran nchini na Syria na Iraq. BBC.

> **Kundi la SDF ambalo lilisaidia muungano unaoongozwa na Marekani kushinda kundi la Islamic State Mashariki mwa Syria, liliongeza kuwa uchunguzi wa awali uligundua kuwa wanamgambo wanaoungwa mkono na Iran.**

# Miaka 60 ya Msondo



Nuta Jazz Band

Na Kaisi Mussa Kaisi

MARA baada ya kupatikana kwa Uhuru, kuliundwa bendi iliyopewa jina la NUTA Jazz ambayo ni kongwe miongoni mwa bendi zilizokuwepo hapa nchini.

Mwaka huu ni takribani miaka 60 tangu ianzishwe mwaka 1964 katika jiji la Dar es Salaam, ikiwa chini ya ummiliki wa Jumuiya ya Wafanyakazi Tanzania (National Union of Tanzania) kwa kifupi NUTA.

Mwaka huohuo wa 1964 Muhidini Gurumo aliitwa kujiunga na bendi hiyo ya hiyo akitokea katika bendi ya Rufiji Jazz, na kuwa mmoja wa waasisi wa bendi. Gurumo aliungana na wanamuziki wengine akina Hamis Sama, Mnenge Ramadhani, Wilfred, Boniface na wengine.

Muhidin Maalim Gurumo nyimbo zake za kwanza kurekodi akiwa na NUTA Jazz zilikuwa Baba Nyerere, uliokuwa ukimsifia Mwalimu Nyerere kwa kuleta Uhuru wa Tanganyika. Nyingine zilikuwa Kilimo ni kazi yetu na Mwengele.

Mwaka 1966 mwanamuziki mwingine mahiri John Simon alijiunga na bendi hiyo ya NUTA Jazz.Mpiga gitaa la solo Amed Omar ndiye aliyechaguliwa kuwa kiongozi wa bendi.

Jumuiya hiyo ilipobadili majina kuwa 'Organization of Tanzania Trade Unions' kwa kifupi OTTU, bendi nayo ikawa OTTU Jazz. Baada ya kipindi kingine kupita Jumuiya hiyo ikabadili majina kuwa Jumuiya ya Wafanyakazi Tanzania, kwa kifupi JUWATA.

Wakati wa uhai wake marehemu Gurumo aliwahi kusema kuwa mpiga solo Ahmed Omar kuwa ndiye aliyechaguliwa kuwa kiongozi wa NUTA Jazz wakati huo.Mzee Gurumo ambaye ndiye aliyekuwa muasisi wa mtindo wa Msondo, ukiwa ni wa asili ya kabila la Kizaramo, aliweza kutamba katika nyimbo.

> **Ushindani kati ya bendi za muziki wa dansi ulipoongezeka mwaka 1978 Muhidini Gurumo na Hassan Reheni Bichuka walihamia bendi ya Mlimani Park Orchestra. Gurumo alipofika katika bendi hiyo akawa kiongozi.**

Baadhi ya nyimbo zilizorekodiwa wakati huo, Mpenzi Sofia, Tumeishi toka zamani, na Walinicheka. Zingine zilikuwa Aziza, Tukiwa na Monica shuleni, Sakina, Maneno ya Nyerere, Mipacha Ngui na nyingine nyingi.

Wakati huo huo mpiga gitaa la solo Saidi Mabera alichaguliwa kuwa kiongozi wa bendi hiyo. Baadhi ya wanamuziki waliounda Juwata Jazz ni pamoja waimbaji Muhidini Gurumo, wengine ni Hassan Rehani Bichuka, na mpiga kinanda Waziri Alli ambaye hivi sasa ni marehemu pia, baadae alikuwa muhimili katika bendi ya The Kilimanjaro Band (Wana Njenje).

Waziri kabla ya kujiunga katika bendi hiyo, alikuwa katika bendi ya taarabu ya Lucky Star ya mjini Tanga. Alifika katika jiji la Dar es Salaam akiwa na nia ya kwenda nchini Marekani kujifunza muziki. Juhudi zake hazikufanikiwa akapelekwa na nduguze kwenda kujiunga katika bendi hiyo. Alipotuwa alikabidhiwa kupiga Kinanda.

Miaka hiyo ya 1980 hadi 1990, takribani kila bendi ilikuwa na wapiga vinanda. Ikumbukwe katika bendi ya Maquis du Zaire alikuwa akibofya Mbuya Makonga 'Adios. Alikuwepo mwanamama pekee Asia Darwesh aliyekuwa akikipapasa kinanda hususani katika bendi ya MK Group, iliyokuwa ikipiga muziki wake katika ukumbi wa Bandari Grill kwenye hotel ya New Africa ya jijini Dar es Salaam.


Vijana Jazz walikuwa na Hassan Shaw, ambaye hivi sasa yupo Ughaibuni akipiga muziki katika kumbi mbalimbali za Kitalii. Bima Lee Orchestra walikuwa na Kassimu Magati wakati Abdul Salvador 'Father Kidevu' alikuwa akipata 'ulaji' ala hiyo.

Ushindani kati ya bendi za muziki wa dansi ulipoongezeka mwaka 1978 Muhidini Gurumo na Hassan Reheni Bichuka walihamia bendi ya Mlimani Park Orchestra. Gurumo alipofika katika bendi hiyo akawa kiongozi wa bendi sanjari na kuasisi mtindo wa 'Sikinde ngoma ya ukae'. Mtindo huo ambao aliwahi kuelezea ni wa asili ya ngoma za kabila lake la Kizaramo.

Baada ya muda mfupi Hassani Bichuka naye aliindoka bendi hiyo Juwata kwenda kuungana na Gurumo katika bendi ya Mlimani Park Orchestra.

Baada ya Bichuka kupondoka, uongozi ukamchukuwa mwimbaji aliyekuwa akishabihiana naye kwa sauti, Shaban Dede 'Kamchape' alikitokea katika bendi ya Dodoma International ya mjini

>> inaendelea uk. 21



Muhidin Maalim Gurumo

# Miaka 60 ya Msondo Ngoma

>> inatoka uk. 20

**Wakati huo ilikuwa katikati ya wimbo wapenzi na mashabiki wa Msondo walikuwa wakiimbishwa kibwagizo cha "Msondo yee Msondo aaa..." wapenzi na walikuwa wakiitikia "Afyaaaa". Bendi hiyo ilikuwa ikipiga muziki wake katika ukumbi wa Amana uliopo Ilala jijini Dar es Salaam, ikipakana na hospitali ya Amana.**




Dodoma wakati huo, sasa ni jiji.

Gurumo alirejea tena katika bendi yake ya Juwata mwaka 1991, akapewa wadhifa wa kuwa kiongozi wa bendi hiyo, baada ya kupiga muziki katika bendi hiyo ya Mliamani Park Orchestra pamoja na Orchestra Safari Sound (OSS) kwa nyakati tofauti.

Nyimbo walizotoka nazo zilikuwa za Nidhamu ya kazi, Ete, Queen Kasse, Mariamu ninakujibu, Usia wa baba, Msafiri kafiri, Tupa tupa, Ndugu Kassimu na nyingine lukuki.

Baadaye bendi hiyo ilibadilishwa jina na kuwa OTTU Jazz kufuatia kubadilika kwa jina la Chama cha Wafanyakazi kuwa OTTU. Hakuna ubishi kwamba bendi ya OTTU Jazz au kwa jina lingine wakajiita 'Baba ya Muziki', ilitikisa jiji la Dar es Salaam na nchi nzima kwa ujumla wakipigia kwa mtindo wa wa 'Msondo Ngoma, magoma Kitakita' au 'Mambo hadharani'.

Wakati huo ilikuwa katikati ya wimbo wapenzi na mashabiki wa Msondo walikuwa wakiimbishwa kibwagizo cha "Msondo yee Msondo aaa..." wapenzi na walikuwa wakiitikia "Afyaaaa".Bendi hiyo ilikuwa ikipiga muziki wake katika ukumbi wa Amana uliopo Ilala jijini Dar es Salaam, ikipakana na hospitali ya Amana.

Katika kipindi hicho bendi hiyo ilikuwa imesheheni wengi wenye vipaji vinavyotofautiana, Wanamuziki hao walikuwa akina Joseph Lusungu, Mnenge Ramadhani, Muhiddin Maalim, Hassan Rehani Bitchuka, Saidi Mabera na TX Moshi William. Wengine ni pamoja na

Nicko Zengekala, Selemani Mbwembwe, Joseph Maina, Mustapha John Ngosha, Suleimani Mwanyiro 'Computer', Tino Maselenge (Masinge) 'Arawa' na Athuman Momba.

Abdull Ridhiwan Pangamawe, Roman Mng'ande 'Romario'

Wengine ni Salehe Bangwe 'mwana Kigoma', na bila kuwasahau Huruka Uvuruge na mzee mzima Said Mabera mpiga solo mahiri ambaye tangia ajiunge katika bendi hiyo hajathubutu kuondoka.

Kufuatia Hospitali ya Amana Ilala kupanuka OTTU Jazz walitakiwa kuondoka kwa kile kilichodaiwa ni kuwabughudhi wagonjwa kwa makelele ya vyombo vya muziki wao hivyo walilazimika kuhamia katika ukumbi wa AfriCenter uliopo barabara ya Kigogo ambako nako hawakudumu kipindi kirefu na hivi sasa wanapiga muziki wao katika ukumbi wa Max Bar uliopo Ilala Bungoni.

Baadhi ya nyimbo zilizogongwa na OTTU Jazz zilikuwa za Kicheko, Mawifi mnanionea, Ndoa Ndoana, Nimezama katika dimbwi, Mti mkavu na Mizimu.

Zingine ni Wabakaji, Tabu, Pricila, Penzi la mlemavu, Piga ua talaka utatoa, Tuma, Wapambe, Asha mwana Sefu, Ajali, Mtanikumbuka, Barua ya kusikitisha, Mwana mkiwa, Kalunde, Kaza moyo, Jesca, Kwenye penzi, Binti maringo, Dalili na nyingine nyingi.

Chama cha Wafanyakazi Tanzania baadaye kijiondoa katika ufadhili wa bendi hiyo, kikawaachia vyombo wajitegemee. Walijikusanya kutengeneza mikakati na kuamua kuipa jina la bendi kuwa Msondo Ngoma ikiwa imesheheni wanamuziki wengi wakiwemo wa zamani na wapya.

Msondo Ngoma ilikuwa na jumla ya wanamuziki 18 na fundi mitambo mmoja. Kiongozi wao alikuwa Said Mabera ambaye pia ni mpigaji wa gita la Solo. Waimbaji wa bendi hiyo ni akaina Juma Katundu, Fresh Jumbe, Shaaban Dede, Twaha Mohamed, Hassan Moshi William 'TX Junior' na Hussein Kalembo.

Wakung'utaji magita ni akina Abdull Ridhiwani Pangamawe ambaye ni bingwa wa kupiga kinanda, Solo na Rhythm, Huruka Uvuruge naye pia ni mpigaji wa Solo na Rhythm, Kassimu Mponda, Mustafa Hamis 'Pishuu' na Zahoro Bangwe wakicharaza gitaa la rhythm.

Kwa upande wa gita zito la besi wapo Ally Lindunga na Saad Ally 'Sure Boy'. Drums huchanganywa na Saad Ally 'Mashine' na Arnold Kang'ombe.Tarumbeta hupulizwa na kijana machachari Roman Mng'ande 'Romari' na Hamis Mnyupe.Dorice George hupiga Tumba, ambaye pia ni Mwimbaji wakati Amiri Said Dongo naye ni mpigaji wa Tumba.

Mtunzi na mwimbaji mahiri Shabani Dede 'Kamchape' alirejea tena katika bendi hiyo akitokea bendi ya Mlimani Park Orchestra 'Wana Sikinde'. Talanta za kutunga na kuimba za marehemu TX Moshi William, ambaye inasemekana yeye ndiye alikuwa mtunzi mkuu katika bendi hiyo kwa wakti huo.

Inaaminika kuwa katika albamu moja waliokuwa wakiifyatua, TX alikuwa katunga nyimbo 8 hadi 9 wakati zilizobaki zinatungwa na Jumuiya.

Tofauti kabisa na miaka ya nyuma upinzani kati ya bendi za Mlimani Park na Msondo Ngoma uliokuwa ukishihudiwa nyakati zile umepungua kwa kiasi kikubwa. Bendi hizo hufikia kuandaa siku ya kupiga muziki kwa pamoja katika viwanja vya TTC Chang'ombe, jijini Dar es Salaam.

Bendi ya Msondo Ngoma music band bado ipo ikiwa na makao yake katika baa ya Dimax iliyopo Ilala jijini Dar es Salaam. Baadhi ya wanamuziki wanaotajwa katika makala hii wamekwisha tangulia mbele za mungu akiwemo Mzee Muhidini Gurumo.

Wengine ni TX Moshi William, Nicko Zengekala, Selemani Mbwembwe, Joseph Mahina, Hamis Kitambi, Mustafa John Ngosha, Suleiman Mwanyiro, Tino Maselenge(Masinge) 'Arawa', Athuman Momba na wapulizaji wa saxophone Mnenge Ramadhani na Alli Rashidi aliyefariki dunia siku ambayo bendi hiyo ikitimiza miaka 50, Oktoba 10, 2014.




TX Moshi William

**Bendi ya Msondo Ngoma music band bado ipo ikiwa na makao yake katika baa ya Dimax iliyopo Ilala jijini Dar es Salaam. Baadhi ya wanamuziki wanaotajwa katika makala hii wamekwisha tangulia mbele za Mungu.**

# Nyota wadogo waliokimbia timu za AFCON na kucheza Ulaya




**Na Valensi Mbaga**

AFRIKA ina utajiri wa vipaji vya soka ambavyo ligi za kigeni zimekuwa zikiibua kwa miongo kadhaa iliyopita na mpaka sasa.Wachezaji kama George Weah, Samuel E'too, na Didier Drogba wamefikia mbali zaidi na kupata mafanikio makubwa na kuleta fahari kwa nchi zao za asili.

Kwa Sasa wachezaji vijana zaidi wa soka barani Afrika wanabadili utii wao kwa nchi asilia kwao. Hii inamaanisha wanaacha nafasi ya kuwakilisha nchi zao za asili kwenye mashindano ya kimataifa. Lakini inaweza kuwa sababu gani?

Wafuatao ni wachezaji wa soka wa Kiafrika bado wanazingatia chaguzi zao na huenda wasicheze kamwe kwa timu za taifa za Afrika

### 5: Bukayo Saka

Timu ya taifa ya Nigeria huenda isifaidike kamwe na huduma za winga huyu mwenye kipawa kikubwa. Saka alizaliwa na kukulia nchini England na tayari amepata majukumu ya klabu na timu ya taifa katika nchi yake ya kuzaliwa. Mnamo 2018 alijitokeza kwa Arsenal kama mchezaji wa akiba katika mchezo wa Ligi ya Europa na polepole anakuwa mchezaji wa kawaida kwenye kikosi cha kwanza. Saka amepitia safu ya vijana ya timu ya taifa ya Uingereza. Mnamo Oktoba 2020 alipata mechi yake ya kwanza katika ushindi wa kikosi cha wakubwa dhidi ya Wales.

### 4: William Saliba

Saliba alianza kucheza mpira wa miguu akiwa na umri wa miaka 6 tu na alifundishwa na baba yake Kylian Mbappe. Mchezo wake wa kwanza alikuwa katika upande wa Ufaransa Saint Etienne mnamo 2018 alipokuwa na umri wa miaka 17.

Julai 2020 alisaini mkataba wa muda mrefu na Arsenal. Mkataba wake ulimweka kwa mkopo Saint Etienne hadi mwisho wa msimu wa 2019-2020. Mchezaji huyu wa soka wa Kiafrika sasa anavaa jezi namba 4 katika klabu ya Arsenal na Licha ya urithi wake wa Cameroon, Saliba amechagua kuichezea Ufaransa na ameshiriki sana katika ligi za vijana.



### 3: Eduardo Camavinga

Camavinga huenda wakawa ndio jina liliopanda zaidi katika safu ya kiungo ya Real Madrid kwa sasa. Raia huyo wa Ufaransa mzaliwa wa Angola anaibuka kuwa mmoja wa wachezaji wa kufurahisha zaidi katika soka la dunia akiwa na umri mdogo.

Mnamo Agosti 2020, Camavinga alikua mmoja wa wachezaji wenye umri mdogo zaidi kupata kuitwa katika timu ya taifa akiwa na umri wa miaka 17. Alichukua nafasi ya Paul Pogba ambaye, wakati huo, hakuweza kucheza baada ya kupimwa na kuambukizwa COVID19. Kuvaa jezi ya Ufaransa kunamaanisha kwamba Camavinga hawezi tena kuichezea congo alikozaliwa mzazi wake au Angola alikozaliwa yeye.

### 2: Adama Traore

Traore alizaliwa Barcelona lakini wazazi wake ni kutoka Mali na ana kaka yake Moha ambaye anacheza soka ya kulipwa nchini Uhispania. Winga huyo mkali amevutia hisia za wachambuzi wa soka tangu enzi zake katika programu ya vijana ya FC Barcelona. Kwa sasa ndiye kinara katika klabu ya Ligi Kuu ya Uingereza Wolverhampton Wanderers.

Mwaka 2014 iliripotiwa kuwa Traore na Moha wameamua kuchezea timu ya taifa ya Mali. Hili halikuthibitishwa rasmi na katika mahojiano ya baadaye, Traore alidai kuwa hakuwa na uamuzi kuhusu kazi yake ya kimataifa.

### 1: Ansu Fati

Ansu Fati ni mchezaji anayechipukia wa soka wa Kiafrika ambaye alizaliwa nchini Guinea-Bissau. Walakini, alihamia Uhispania na familia yake wakati alikuwa na umri wa miaka 6. Baba yake Bori Fati aliichezea timu ya taifa ya Guinea-Bissau kisha akahamia Ureno na baadaye Uhispania ambapo Ansu alitumia muda mwingi wa miaka yake ya malezi. Ansu alichezea timu za vijana huko Sevilla kabla ya kujiunga na akademi ya vijana ya Barcelona alipokuwa na umri wa miaka 10 tu.



Hapo awali Ansu alistahili kuichezea Guinea-Bissau lakini hakuchukua hatua zozote kutimiza wajibu wake wa kitaifa kwa mahali alipozaliwa. Baada ya kuonekana kwa kilabu kwa Barcelona, timu ya kitaifa ya Uhispania ilianza kuonyesha nia. Kwa kuwa Ansu pia alistahiki pasipoti ya Ureno kutokana na uhusiano wa Guinea Bissau na Ureno, Uhispania ilimpa uraia haraka. Katika mchakato huo, ilimbidi kuukana uraia wa mahali alipozaliwa

Hatuwezi kuwalaumu wachezaji wa soka wa Kiafrika kwa kubadili utaifa waona kutimka nchi za Ulaya. Ikiwa vyama vya soka vya Afrika vingewapa jukwaa la kujiendeleza, wengi wao wangebaki Afrika. Ligi zinazoaminika na zenye ushindani, malipo mazuri, na nafasi katika timu ya taifa ni baadhi ya njia Afrika inaweza kuweka vipaji vyake vya vijana. Je, unadhani kuna hatua nyingine ambazo nchi za Afrika zinaweza kuchukua kulinda vipaji vyao vya soka?

# Kona ya Urembo



Na Hidaya Machuppa Simu: +255 765 828 219

# Tokelezea ufukweni
















**Suala la mavazi ya pwani kwa wanaume, kuna mitindo mbalimbali ambayo hivi karibuni imekuwa maarufu. Mionekano hii inachanganya starehe.**



MAVAZI ya pwani kwa wanaume ni kitu ambacho kinaweza kufanywa kwa kuchanganya na nguo. Haya hapa ni mawazo machache ya kutengeneza mashati yako ya Kihawai, na kaptura za rangi ya pastel, ili utakapokuwa ufuoni tena, uonekane 'wakushangaza'

Linapokuja suala la mavazi ya pwani kwa wanaume, kuna mitindo mbalimbali ambayo hivi karibuni imekuwa maarufu. Mionekano hii inachanganya starehe, utendakazi, na muundo ili kutoa mwonekano mzuri na wa kustarehesha unaofaa kwa siku moja ufukweni wakiwa wamevaa wanaume. Mavazi kama;

**Shorts za kuogelea:** Hizi ni za msingi na mojawapo ya mitindo ya kuogelea ya wanaume. Zinapatikana kwa urefu mbalimbali kutoka juu ya goti hadi katikati ya paja, pamoja na aina mbalimbali za rangi na miundo. Machapisho ya maua, mifumo ya kijiometri, na rangi angavu ni maarufu sana.

**T-shirt zilizo na chapa:** T-shirt zilizo na chapa ni chaguo la kufurahisha na lisilo rasmi ambalo limekuwa likijitokeza kama mitindo ya mavazi ya ufukweni ya wanaume kwa ufuo. T-shirt zilizo na mwelekeo wazi, motifs za kitropiki, au miundo ya ujasiri ya picha ni bora. Ili kufanya t-shati ionekane, iunganishe na kaptula za rangi zisizo na rangi au shina za kuogelea.

**Mashati ya kitani:** mashati haya huwa na vifungo na mepesi sana,haya paswi kubana wala kuachia sana ambayo inafaa mtindo wa majira ya joto. Wanatoa mtindo mzuri zaidi wakati wa kustarehesha. Kwa sauti ya pwani, chagua tani nyepesi au nyeupe.



Vitu Muhimu Unavyohitaji katika Mavazi Yako ya Ufukweni.

**Ulinzi wa Jua:** Mavazi yoyote ya ufukweni kwa wanaume unayovaa, ni muhimu kulinda ngozi yako kutokana na miale hatari ya jua. Usisahau kujumuisha vitu vifuatavyo vya kujikinga na jua hata kama unavaa nguo za kiume.

**Kinga ya jua:** Ili kulinda ngozi yako dhidi ya mionzi ya UVA na UVB, tumia mafuta ya kukinga jua yenye viwango vya juu vya SPF. Inapaswa kutumika tena kila masaa kadhaa, haswa baada ya kuogelea.

**Miwani ya jua:** Miwani ya jua ni muhimu kwa mavazi ya pwani ya wanaume. Inasaidia kulinda macho yako kutokana na jua, wekeza kwenye jozi ya miwani ya jua iliyolindwa na UV. Tafuta mitindo ambayo hutoa ufunikaji wa kutosha na inayosaidia umbo lako la uso.

**Kofia maridadi ya Ufukweni:** Je! huna uhakika wa kuvaa vifaa vya mtindo wa watu wa pwani? Kofia ya ufukweni ya mtindo sio tu inakulinda kutokana na jua lakini pia inaongeza mguso wa hali ya juu kwa mtindo wako. Ili kuunda kauli ya maridadi, vaa kofia ya majani yenye ukingo mpana, kofia ya jua inayopeperushwa, au kofia ya mtindo wa fedora. Kwa mtindo ulioongezwa, chagua kofia zilizo na mapambo kama vile riboni, bendi za rangi, au vipengee vilivyo na muundo.



**Kofia:** kofia yenye ukingo mpana ili kulinda uso, masikio, na shingo yako kutokana na jua moja kwa moja huifanya kuwa mojawapo ya mtindo wa lazima wa ufukweni wa wanaume. Kofia ya majani au kitambaa cha UPF (Ultraviolet Protection Factor) ni chaguo bora kwa safari za pwani.

**Taulo ya ufukweni:** Taulo kubwa la ufukweni, linalofyonza linahitajika kwa kulala kwenye mchanga au kukauka baada ya kuogelea. Ili kuongeza umaridadi kwa mwonekano wako wa ufukweni, chagua taulo zilizotengenezwa kwa nyenzo laini, zinazokausha haraka na uzingatie rangi nzito au miundo ya kufurahisha.

**Sandals:** Iwe ni vazi lolote la ufukweni kwa wanaume, viatu vya starehe ni muhimu, na flip-flops au viatu ni chaguo la kwenda kwenye nguo za wanaume. Tafuta njia mbadala ambazo hazina maji na zina mshiko mzuri na usaidizi wa upinde. Chagua mifumo ambayo ni rahisi kuteleza,na kuifanya iwe bora kwa mipangilio ya mchanga.

**Vidani na kacha:** Kuvaa mavazi ya ufukweni kwa wanaume kunaweza kufanywa kwa kutumia shanga zenye safu au vikuku vilivyopangwa ambavyo vinatoa msisimko. Chagua vito maridadi vya ufuo kama vile shanga za ganda, vikuku vilivyo na shanga na mikufu ya mtindo wa kamba. Kuchanganya urefu na textures tofauti ili kuunda seti ya kipekee na ya kuvutia macho.

Kuzingatia muonekano wa ufukweni ni vizuri zaidi ili kuendana na mazingira na usasa zaidi.Utashangaza dunia pale utakapoonekana na suti ufukweni.Kama ilivyo ufukweni ni sehemu ya kubarizi basi fanya watu wakubarizi kwa kukuangalia

Leo yetu ndiyo kesho yetu

# Uelekeo Spoti

| Jumatano Februari 07-13, 2024 |

## Aliyemsajili Mayele atimuliwa Pyramids

**Na Mwandishi Wetu**



KOCHA Jamie Pacheco wa timu ya Pyramids ya nchini Misri ameachana na klabu hiyo kwa makubaliano ya pande mbili.

Pyramids katika taarifa yao kuwa wamekubaliana pande zote mbili ya kuvunja mkataba huo.

Pacheco ndiye aliyetoa mapendekeza ya kumsajili Fiston Kalala Mayele kutoka Yanga.




# Simba 4G

**Na Mwandishi Wetu**

MNYAMA hana huruma amevunja masega yote ya asali na kuilamba mara nne.

Simba bado iko nafasi ya tatu kwa kufikisha pointi 29 ikiwa nyuma ya Azam na Yanga wanaoongoza ligi.

Katika pambano lililofanyika Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi, Simba ilionekana ni mlima mkubwa sana kwa Tabora United.

Mabao manne yaliyofungwa na Sadio Kanoute, Omari Jobekatika kipindi cha kwanza na Chemalone Conde na Fred Michael wakiimarisha mnara wa 4G.

Leo Yanga wanashuka Chamazi kwa kumenyana na Mashujaa ya Kigoma ambayo ilipokea kipigo cha bao 1-0 kutoka kwa Simba siku chache zilizopita.

# Mume wa mtu amponza Miss Japan

**Na Mwandishi Wetu**

MISS Japan 2024 Karoline Shiino amepoteza taji hilo baada ya kubainika kuwa kwenye mahusiano ya kimapenzi na mume wa mtu.

Shino ambaye ni mzaliwa wa Ukraine amejivua taji lake baada ya ripoti kufichua uhusiano wake na mwanamume huyo.

Shiino mwenye umri wa miaka 26, alitawazwa kuwa 'Miss Japan' wiki mbili zilizopita lakini ushindi wake ulizua mjadala wa umma kutokana na asili yake.

Wakati wengine wakibariki ushindi wake kama raia halali wa nchi hiyo, wengine walisema hakuwakilisha maadili ya kitamaduni ya urembo ya Kijapani.

Wakati hayo yakijiri jarida moja la eneo hilo lilifichua kuwa mlimbwende huyo alikuwa kwenye uhusiano wa kimapenzi mwanaume aliyeoa ambaye ni mshawishi na Daktari ingawa mwanaume huyo hajazungumza lolote kuhusiana na sakata hilo.

Katika ripoti ya awali waandaaji wa shindano hilo walimkingia kifua Shiino wakidai kuwa mrembo huyo hakujua kuwa mwanamume huyo alikuwa ameoa.

Hata hivyo baadaye waandaaji hao waliweka wazi kuwa Shiino amekiri kufahamu kuhusu ndoa na familia ya mwanamume huyo.

"Alikuwa ameomba radhi kwa kupotosha na waandaaji walikubali kujiuzulu kwa taji lake," Chama cha Miss Japan kilisema.

Mlimbwende huyo aliwaomba radhi mashabiki wake na umma kwa ujumla katika taarifa yake siku ya Jumatatu, ambapo alisema ametenda kwa woga na hofu wakati wa kutoa majibu kuhusu ripoti hiyo.

"Ninasikitika sana kwa shida kubwa niliyosababisha na kuwasaliti wale walioniunga mkono," alisema.

Taji la Miss Japan sasa litakuwa wazi hadi msimu ujao.

Shiino alitawazwa kuwa Miss Japan Januari 22 mwaka huu akiwa ni mtu wa kwanza mwenye asili ya Ulaya kupewa heshima hiyo.

Alizaliwa Ukraine kabla ya kuhamia Japan na mama yake wakati huo akiwa na miaka mitano na kuchukua jina la mwisho la baba yake wa kambo wa Kijapani.



## Kivumbi nusu fainali AFCON

**Na Mwandishi Wetu**

USIKU wa deni siku zote haukawii kukucha iwe kwa mdai au mdaiwa na hii ndivyo ilivyo nchini Afrika Kusini.

Roho za mashabiki wa soka Afrika zimeelekezwa nchini humo ambapo miamba minne inashuka dimbani kutafuta nafasi ya kuchukua ufalme Tanzania.

Bafana Bafana ambayo wengi wanaichukulia kama Brazil ya Afrika kutokana na aina ya soka lao huku timu hiyo ikuundwa na wachezaji wengi kutoka mabingwa wa Kombe la AFL, Mamelod Sundowns.

Bafana watakuwa wanabiliana na Nigeria ambao wanahitaji ubingwa wa tisa wa Afrika.

Lakini shughuli pevu iko kwa wenyeji na mabingwa watetezi Ivory Coast ambao watakabiliana na wana Kibinda Nkoi Congo DR.

Ivory Coast wameweza kuvuka kiunzi cha michuano ya miaka 10 nyuma ambapo bingwa mtetezi ameshindwa kuvuka hatua ya robo fainali.


Kimzani mechi zote hazitabiriki lakini zote kali.



## AFCON sasa kuwa Juni

**ABIDJAN, Ivory Coast**

SHIRIKISHO la Soka Afrika (CAF) limebadilisha ratiba ya michuano ya Mataifa Afrika (AFCON) kuanzia ya mwakani.



CAF sasa imepanga AFCON kuchezwa mwezi Juni na sio Januari ili kutoa nafasi kwa ligi kumalizika.

Morocco ndiyo waandaaji wa mashindano hayo yajayo.

CAF imesema pamoja na kumalizika kwa ligi lakini mashindano yakifanyika mwezi Juni yatatoa nafasi kwa watu wengi duniani kuyafuatilia.